
www.umg.co.tz

Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Mweleko



JAMII

UK.11

## UCHUMI

**TPDC na uwekezaji mkubwa miaka miwili ya Dk. Samia**

Uk. 8





MICHEZO

**Simba yatamba kwenda nusu fainali Klabu Bingwa**

Uk.24

Toleo Na. 00005

| Jumatano Machi 15 - 21, 2023 |

umgdigital umgdigital mweleko@umg umgdigital

MIAKA MIWILI DK. SAMIA MADARAKANI:

# 'Bwawa la Nyerere, SGR viliniumiza akili'

HABARINDANI

## NHC yazidi kujitanua




Uk. 3



## Athari za kuangalia runinga

Uk. 15



Uk. 4

## 'Ushoga na dhana ya kuoana'

Uk. 10

# Wanasayansi Tanzania, India 'kukuna vichwa' dawa za mbu

**Na Mwandishi Wetu**

WANASAYANSI wa Taasisi ya Afya Ifakara mkoani Morogoro, wataungana na wenzao wa nchi nyingine tatu duniani katika kufanya tathmini ya viuatilifu vya kuzuia mbu wanaoeneza malaria.

Viatilifu hivyo ni vile wanavyowekwa kwenye vyandarua ambavyo hata hivyo, imebainika kuwa mbu wamekuwa na uwezo mkubwa wa kuvikabili kuliko ilivyotarajiwa.

Wanasayansi wengine katika utafiti huo watatoka India na Ivory Coast na tathmini watakayoifanya itahusisha viatilifu vya Veerali, Tsara boost na Olyset Plus.

Taarifa ya utafiti iliyowekwa kwenye tovuti ya Taasisi ya Afya Ifakara, inasema hatua hiyo inalenga katika kutafuta ufumbuzi kuhusu upinzani wa mbu wanaoeneza malaria dhidi ya viatilifu vinavyowekwa kwenye vyandarua.

"Wanasayansi hao wanatazamiwa kufanya majaribio kwa wakati mmoja juu ya viuatilifu vitatu ambavyo ni Veeralin, Tsara Boost na Olyset Plus dhidi ya pyrethroid-PBO," inasema sehemu ya taarifa.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, vyandarua vina msaada mkubwa katika vita dhidi ya malaria katika kampeni ya matumizi yake iliyofanywa na serikali, lakini dawa za kufukuza mbu zinazowekwa kwenye vyandarua hazijaleta matokeo yaliyotarajiwa na ya muda mrefu.

"Juhudi zilizofanikiwa za kutumia vyandarua ziko hatarini kwa kiasi fulani kutokana na kuongezeka kwa upinzani wa mbu dhidi ya kiuatilifu… muda wa kuishi wa vyandarua ni mfupi," ilisema.

"Katika jitihada za kutafuta ufumbuzi wa changamoto hizi, kundi la watafiti kutoka nchi tatu wakiwamo wa Ifakara, wanatazamiwa kufanya majaribio kwa wakati mmoja juu ya viuatilifu vitatu katika chini za Tanzania, India na Ivory Coast," iliongeza taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa, jaribio hilo litapima uimara wa pyrethroid-PBO kama inakidhi viwango vya Shirika la Afya Duniani (WHO), kuhusu ufanisi wake wa miaka mitatu unaolenga kukitambua kama kiuatilifu kinafanya kazi kwa muda mrefu.

Taarifa ilisema ufuatiliaji wa uwezo wa dawa hiyo, utafanyiwa tathmini kwa kipindi cha hadi miaka mitatu baada ya usambazaji na kwamba hapa nchini, tathmini hiyo itafanyika Ifakara.

Ilisema utafiti utakuja na majibu kuhusu muda wa kujazwa tena dawa kwa vyandarua vilivyowekwa dawa ya PBO.

Wanasayansi wa Taasisi ya Ifakara watakaoungana na wale wa kigeni katika utafiti huo ni, Emmanuel Mbuba, Olukayode Odufuwa, Jason Moore, Selemani Mmbaga na Sarah Moore.

# TGNP yawafunda mabinti picha za utupu mitandaoni

**Na Mwandishi Wetu**

MTANDAO wa Jinsia Tanzania (TGNP), umewafunda wanawake na mabinti kuhusu matumizi sahihi ya teknolojia ukiwaasa kutorekodi na kutuma mitandaoni picha za utupu kwani zinasababisha unyanyasaji kwa wanaume.

Akizungumza kwenye maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa TGNP, Lilian Liundi, alisema picha za utupu zinachochea ukatili kwa watoto wa kiume na wanaume kwa ujumla.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, akizungumza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mwanamke Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya mtandao huo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki iliyopita. (Picha: Mpigapicha Wetu)

Katika maadhimisho hayo ambayo yaliongozwa na kaulimbiu ya 'Jinsia na Teknolojia: Ubunifu na Mabadiliko ya Teknolojia chachu ya Usawa wa Kijinsia', Liundi alisema picha hizo ni kikwazo cha kupata kazi au nafasi nzuri siku zijazo.

"Badala ya kutumia teknolojia, hasa mitandao ya kijamii kufanya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia, nitoe hamasa kwa jamii kutumia teknolojia hii kuelimisha jamii kuachana na vitendo hivyo na kuchukua hatua ili kuvitokomeza," alisema.

Aidha, alitoa rai kwa wanasayansi na teknolojia kuja na uvumbuzi wa vifaa vitakavyosaidia katika harakati za kutokomeza ukatili wa kijinsia.

Kwa upande wake, bingwa wa Hisabati, Profesa Veridiana Masanja, alitaja mbinu za kukabiliana na ukatili wa kijinsia mtandaoni kuwa ni kuitumia kama zana ya kutoa elimu na kukemea udhalilishaji.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, alisema mitandao ya kijamii ni nyenzo muhimu ya kukabiliana na vitendo vya kikatili.

"Jamii inaweza kukemea na kutoa taarifa mbalimbali juu ya matukio ya ukatili wa kijinsia, kuchukua hatua stahiki katika muda muafaka na pia kuelimisha na kuhamasisha jamii dhidi ya ukatili wa kijinsia," alisema.

> **Jamii inaweza kukemea na kutoa taarifa mbalimbali juu ya matukio ya ukatili wa kijinsia, kuchukua hatua stahiki katika muda muafaka...**

Profesa Masanja alisema wanawake wanaweza kutumia teknolojia kukuza biashara zao kwa kutumia mitandao ya kijamii na kuboresha vipato vyao na kwamba hilo linawezekana kwa kuwa upatikanaji wa taarifa na maarifa umerahishishwa.

Hata hivyo, alisema licha ya fursa hizo, matumizi ya teknolojia yanachangamoto nyingi ikiwamo unyanyasaji wa kijinsia na utapeli wa kimtandao.

Alisema takwimu za serikali za Machi mwaka jana zinaonyesha kwamba asilimia nne ya watumiaji wa mtandao wenye umri wa miaka 12-17 nchini Tanzania ni manusura wa ukatili wa mitandaoni.

"Tunaomba Serikali iimarishe utekelezaji wa sheria zilizopo na itunge kanuni ambazo zitakuwa na mrengo wa kijinsia kwa ajili ya kutoa ulinzi maalumu kwa watoto wa kike dhidi ya unyanyasaji wa kimtandao," alisema.

Awali katika mkutano huo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TGNP, Gemma Akilimali, TGNP kwa kushirikiana na serikali imetengeneza kanzidata ya kuweka taarifa za wanawake viongozi ili kurahisisha kupatikana kwa taarifa zao kila zinapohitajika.

Alisema mtandao huo kwa kushirikina na Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam (DIT), kimetengeneza kanzidata inayoitwa Tanzania Women Konnect Portal ambayo imejikita katika kuhifadhi kazi za wanawake walio katika nyanja mbalimbali.

# TARURA yaanika sababu barabara Songwe kutopitika

**Na Lauden Mwambona, Songwe**

WAKALA wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) Mkoa wa Songwe, umesema asilimia 70.43 ya barabara zake mkoani humo hazipitiki wakati wa masika kutokana na kuwa za udongo.

Meneja wa Tarura mkoani humu, Mhandisi Killian Haule, aliyasema hayo katika taarifa aliyoiwasilisha kwenye kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Songwe hivi karibuni.

Mhandisi Killian alisema kwa ujumla Tarura inahudumia barabara zenye urefu wa kilomita 3,341.640, lakini kilomita 2,353.502 ni za udongo na za lami ni kilomita 20.326.

Alisema barabara za Tarura zinazopitika wakati wote mkoani Songwe zina urefu wa kilomita 988.128 sawa na asilimia 29.57.

Aidha, alisema mwaka huu wa fedha, Tarura mkoani Songwe imepangiwa zaidi ya Sh. bilioni 21 kwa ajili ya kuhudumia barabara zake.

Naye Meneja wa Tarura Wilaya ya Ileje, Injinia Lugano Mwambingu, alitaja changamoto za kazi ya kutengeneza barabara kwamba ni uhaba wa mitambo ya kazi kutokana na mkoa kuwa mpya.

Alishauri juhudi zifanyike kuhamasisha wadau mbalimbali waweke vituo vya kukodisha mitambo ya kutengeneza barabara mkoani Songwe.

Wakijadili, baadhi ya wajumbe wa Bodi ya Barabara, waliiomba serikali kuendelea kuongezea fedha Tanroads na Tarura Mkoa wa Songwe ili kufungua barabara nyingi zisizopitika wakati wa mvua.

# Mwanafunzi akikutwa ameshika, anavuta bangi shule `bye bye'

**Na Mwandishi Wetu, Bagamoyo**

WANAFUNZI wa Shule ya Sekondari ya Dunda Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani, wakikutwa wameshika au wanavuta bangi, watafukuzwa shule.

Kauli hiyo inayolenga kulinda nidhamu na ufaulu shuleni hapo, ilitolewa na Diwani wa Kata ya Dunda wilayani humu, Amiri Mpwimbwi.

Kadhalika, mwanafunzi atayekutwa na fedha taslim kuanzia Sh. 5,000, atahojiwa kwa kina na ikibidi mzazi wake ataitwa kutoa maelezo kuhusiana na kiasi hicho cha fedha.

Diwani Mpwimbwi alitoa kauli hiyo mbele ya Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wilayani hapa, Mariam Mkali aliyefuatana na viongozi wa kata kutembelea shule hiyo na kuzungumza na wanafunzi mwishoni mwa wiki.

"Shule yetu imeendelea kuwa na wanafunzi wenye nidhamu ya hali ya juu, lakini wapo baadhi yao wanadaiwa kujihusisha na uvutaji wa bangi. Kuanzia sasa, yeyote atayekutwa ameshika au anavuta bangi, tutamfukuza shule," alisisitiza Diwani Mpwimbwi. Kwa upande wake, Mkali aliwaasa wanafunzi hao kuzingatia masomo na kuachana na tamaa za kidunia kwa kuwa hazina mwisho.

Pia aliwashauri wanafunzi kujiepusha na tamaa ikiwemo ya kuomba lifti za usafiri. Naye Mkuu wa Kitengo cha Jinsia Jeshi la Polisi Bagamoyo, Augenia Magwila, alisema katika ofisi yake, kumekuwepo na baadhi ya kesi zinazohusisha wanafunzi kuwashtaki wazazi kwa kukataa kuwasomesha na nyingine za wanafunzi kukataa shule.

## MIAKA MIWILI YA DK. SAMIA:

# NHC yajivunia mafanikio makubwa

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC), linajivunia mafanikio lililoyapata katika miaka miwili tangu Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, aingie madarakani likieleza kuwa sekta ya nyumba imechanua na kukua kwa kasi.

Taarifa ya NHC kuhusu miaka miwili ya Rais Samia ilieleza kuwa katika kipindi hicho, Rais ameliruhusu Shirika kukopa fedha za kukamilisha miradi iliyokuwa imesimama ya Morocco Square, Kawe na Regent Estate.

Ilieleza kuwa kutokana uamuzi huo, Shirika lilipata mkopo wa kiasi cha Sh. bilioni 44.7 kutoka CRDB na NMB ambazo zilitumika kumalizia ujenzi Morocco Square na ule wa Regent Estate.

Ilieleza kuwa, Februari mwaka huu, Wizara ya Fedha imeliruhusu Shirika hilo kukopa fedha za kukamilisha miradi mingine iliyosimama ikiwemo Kawe 711 na mradi mpya wa nyumba za watu wa kipato cha chini na kati wa Samia jijini Dar es Salaam.

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa serikali imeendelea kuchochea mashirikiano kati ya sekta binafsi na sekta ya umma na kuunda idara kamili ya nyumba kwenye Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

"Ujenzi wa nyumba umechanua, uchumi wa Shirika umeongezeka na Shirika limeendelea kufanya majukumu yake ya ujenzi wa nyumba za makazi na biashara kwa ajili ya kuuza na kupangisha," ilieleza taarifa ya NHC.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa Serikali imehakikisha inasimamia kuwapo kwa sera ya nyumba ambayo ndio mwongozo muhimu kwa sekta ya nyumba nchini.

"Kuimarika kwa sekta mbalimbali hususani barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii, huduma za maji, utawala bora, mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi, pamoja na kuhamasisha uwekezaji kuna athari kubwa na chanya kwenye maendeleo ya sekta ya nyumba na makazi nchini," ilifafanua taarifa hiyo.

> **Shirika la Nyumba lina mtaji (capital base) wa Shilingi trilioni 5.04 hivi sasa unaotokana na rasilimali ya majengo yake 2,650 yenye nyumba(Units) zipatazo 18,654 zilizopo katika mikoa mbalimbali nchini...**

Iliongeza kuwa: "Msukumo mkubwa umejikita katika kuhakikisha usimamizi madhubuti wa fedha za umma na kuzielekeza kwenye maeneo yatakayoongeza tija, ajira na kuinua uchumi wa mwananchi mmoja mmoja."

Ilieleza kuwa NHC imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Shirika wa Miaka 10 (2015/16 – 2024/25) ambao unalenga kujenga nyumba 10,000 na kuwezesha ukuaji wa sekta ya nyumba kupitia ushirikishwaji wa sekta binafsi.

"Shirika la Nyumba lina mtaji (capital base) wa Shilingi trilioni 5.04 hivi sasa unaotokana na rasilimali ya majengo yake 2,650 yenye nyumba(Units) zipatazo 18,654 zilizopo katika mikoa mbalimbali nchini," ilisema.

NHC katika taarifa hiyo lilieleza kuwa katika kipindi cha miaka miwili ya Rais Samia madarakani, Serikali ya awamu ya sita ililipatia mkopo nafuu wa Sh. bilioni 20 ili kuongeza kasi ya ujenzi wa nyumba 1,000 jijini Dodoma.

"Fedha hizo zimewezesha ujenzi wa nyumba 404 hivi sasa na Shirika limenunua ardhi maeneo ya Njedengwa ili kuwezesha ujenzi wa nyumba hizo... ruhusa ya Hazina kwa NHC kukopa ambako kumetokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais kutasaidia utekelezaji wa wa Samia Housing Scheme (SHS), utakaowezesha ujenzi wa nyumba 5,000 nchini zitakazogharimu Sh. bilioni 466," ilifafanua.

Ilisema tayari NHC limeanza ujenzi wa nyumba 560 katika eneo la Kawe.

Iliongeza kuwa katika kipindi cha miaka miwili, shirika hilo limeaminiwa na kupewa miradi minane ya Wizara za Serikali inayogharimu Sh. bilioni 106 Jijini Dodoma.

Kadhalika, NHC limepewa miradi ya ujenzi wa Ofisi za Wakala wa Ununuzi na Ugavi Serikalini (GIPSA), yenye thamani ya Sh. 2.8 bilioni itakayojengwa Kibaha, Mtumba- Dodoma, Simiyu na Songwe.

Aidha, Serikali ya awamu ya sita imelipatia Shirika mradi wa Tanzanite Center unaojengwa eneo la Mererani mkoani Manyara wenye thamani ya Sh. Bilioni 5.49 ambao ulianza Mei 2022 na unatarajiwa kukamilika Mei mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, shirika linajenga majengo mengine katika Hospitali ya Ligula mkoani Mtwara. Ujenzi huo ulianza Aprili 2022 na utakamilika Juni, 2023 kwa gharama ya Sh. bilioni 2.7.

# Pinda kuongoza maadhimisho ya Dk. Samia Mbeya



**Na Lauden Mwambona, Mbeya**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya CCM ambaye ni Waziri Mkuu Mstaafu wa awamu ya nne, Mizengo Pinda, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho ya miaka miwili ya uongozi wa mafanikio wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya , Shaibu Akwilombe, aliliambia gazeti hili kwamba maadhimisho hayo yameandaliwa na CCM Mkoa na kwamba yatawashirikisha viongozi mbalimbali wa Serikali, Chama na wabunge.

Akwilombe alisema maadhimisho hayo yataanza Machi 17, mwaka huu yakiongozwa na Pinda kwa kufanya kongamano kubwa litakalojadili mafanikio mbalimbali ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia

Alisema katika kongamano hilo, viongozi wa serikali na wabunge, wanatarajiwa kueleza mambo mbalimbali yaliyofanyika katika maeneo yao na majimbo.

Katibu wa CCM Mkoa alifafanua kuwa Machi 18, mwaka huu, utafanyika mkutano wa hadhara katika viwanja vya Ruanda Nzovwe ambao utahutubiwa na mgeni rasmi, Pinda anayetarajiwa kuwasili mkoani humu kesho.

Alisema wageni mbalimbali wa kitaifa na mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, pia wanatarajiwa kuhudhuria.

Naye Katibu wa CCM Mkoa wa Songwe, Juma Mpeli, alisema CCM Mkoa wamejiandaa kuelekea Mbeya kwa ajili ya maadhimisho hayo.

Mpeli alisema maadhimisho hayo yapo kwenye Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na kwamba pamoja na kushirikisha wageni wa kitaifa, pia wanaCCM wa mikoa ya kanda hiyo watashiriki.

## MIAKA MIWILI DK. SAMIA MADARAKANI:

# `Bwawa la Nyerere, SGR viliniumiza akili'

**Mwandishi Wetu**

MRADI wa Umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, ulimuumiza akili Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, wakati anaingia madarakani miaka miwili iliyopita.

Kiongozi huyo aliingia madarakani Machi 19, mwaka 2021, kufuatia kifo cha mtangulizi wake, Hayati Dk. John Magufuli, ambaye kabla hajafariki dunia, alikuwa ameasisi na kuanza kuitekeleza baadhi ya miradi ya kimkakati.

Rais Samia anasema hali hiyo ilitokana na changamoto mbalimbali zilizokuwa mbele yake ikiwa ni pamoja na kiwango kikubwa cha fedha zilizokuwa zinahitajika kugharimia miradi hiyo muhimu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Hata hivyo, kwa ushupavu na umahiri wake katika uongozi, mwanamke huyo wa 'shoka,' anaendelea kuutekeleza kwa ufanisi mkubwa na kwa viwango vinavyokubalika kimataifa, mradi huo na ule wa reli ya kisasa (SGR).

Wakati Dk. Magufuli akiwa Rais, Dk. Samia ambaye kwa sasa anaendelea kutekeleza na kuhitimisha miradi hiyo, alikuwa Makamu wake wa Rais.

Hivi karibuni wakati akishuhudia utiaji saini wa mikataba 26 ya utekelezaji wa miradi ya umeme katika maeneo ya mijini na vijijini kote nchini, kiongozi huyo Mkuu wa Nchi, alitamka hadharani kuwa wakati anaingia madarakani, kuna miradi ukiwemo mradi mkubwa wa kufua umeme kwa maji katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, ilimuumiza hasa akili yake.

"Wakati mliponikabidhi madaraka, hakuna jambo lililoniumiza akili yangu kama Mradi wa Umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na Reli ya SGR ya kwenda Kigoma, kila nikiangalia mapesa yanayohitajika pale, nikasema Mungu wangu Samia mie nitapata wapi pesa hizi, Mungu nisaidie. Lakini kwa kuwa penye nia pana njia, leo hii SGR nina pesa hadi ya loki ya sita kufika Kigoma, sikutegemea...kwa upande wa Bwawa, nadhani mwakani mapema mapema tunaanza kuiwaisha na kujenereti umeme wa majaribio," alinena.

Mradi mkubwa wa kufua umeme kwa maji katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, utazalisha takribani megawati 2,115 na utagharimu Sh. trilioni 6.5 utakapokamilika. Ni mradi wa nne kwa ukubwa katika miradi ya kuzalisha umeme wa maji Barani Afrika.

Kwa maneno mengine, changamoto hizo na nyingine, hazimkuvunja moyo mwanamama huyo shupavu na mahiri katika uongozi wa kisiasa.

Kwa upande mwingine, ujenzi wa SGR unatarajiwa kugharimu takribani Dola bilioni 1.2 za Kimarekani utakapokamilika.

Baadhi ya wachambuzi wa mambo wamesema mafanikio hayo ya Dk. Samia ambaye ni mwanamke wa kwanza nchini kushika wadhifa wa Urais tangu taifa lilipopata uhuru wake mwaka 1961, yamechangiwa kwa kiwango kikubwa na kuimarika kwa usalama, uchumi unaochochewa na uwekezaji mkubwa katika sekta za kilimo, madini, utalii, ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji na maridhiano ya kisiasa.

Wanasema katika kipindi hicho, Rais Dk. Samia, ametekeleza na anaendelea kutekeleza kwa ufanisi mkubwa mipango mingi ya serikali anayoiongoza na kwamba hiyo ni ishara ya wazi kuwa ataingia katika mwaka wa tatu kwa 'moto mkali'.

"Usalama na amani vinavyoendelea kuimarishwa na serikali yetu, ndiyo vitu vya muhimu sana katika utekelezaji wa haya yote tunayoongea leo kuhusu mambo makubwa yanayofanywa na mama yetu Rais wetu Dk. Samia. Nchi yetu imeendelea kuwa tulivu na kila mtu anafanya mambo yake kwa amani na kujiamini," alisema Rosada Kinjite, alipokuwa akizungumza na gazeti hili.

Rosada ambaye ni mmoja wa watu waliokuwa wakizungumzia miaka miwili ya Rais Samia kuwepo madarakani, alisema mwanamke huyo wa shoka, amefanya mambo mengi ya kimaendeleo yanayostahili si tu kupongezwa, lakini pia yanayowavutia watu wengi ndani na nje ya Tanzania.

Amesema katika kipindi hicho kifupi, Rais ameliwezesha taifa kupiga hatua kubwa za kiuchumi kupitia uwekezaji mkubwa unaoendelea katika sekta za kilimo, madini, utalii na kadhalika.

Rosada aliyekuwa akizungumza kwa njia ya simu, alisema kwa hatua hizo kiongozi huyo wa nchi, ameonyesha dhamira na uzalendo wa kweli wa kuliwezesha taifa na watu wake, kupiga hatua kubwa za kimaendeleo.

Katika uongozi wake, Rais Samia amekuwa akielekeza nguvu kubwa za serikali katika kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati na inayoleta matokeo chanya.

> **Kazi anayopiga mama Samia inaonekana, si kazi ya mchezo, kila kona ukienda kuna barabara safi za lami na nyingine za changarawe, lakini katika kiwango kizuri....**



Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa barabara za lami na changarawe, zinazofungua kanda moja na nyingine, mkoa na mkoa na hata wilaya moja na nyingine.

Ujenzi wa miundombinu hiyo, unalenga kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji wa shehena za mizigo yakiwemo mazao ya kilimo, kwenda kwenye masoko ya kuaminika na hivyo kuwawezesha wakulima kunufaika na shughuli za kilimo.

Kwa mujibu wa hotuba ya bajeti ya ofisi ya waziri mkuu, katika mwaka wa fedha wa 2021/22, serikali imejenga jumla ya kilomita 251.9 za barabara kwa kiwango cha lami zilizohusisha barabara kuu, barabara za mikoa na wilaya.

Lengo ni kuhakikisha kuwa makao makuu ya mikoa yote na nchi jirani zinaunganishwa kwa mtandao wa barabara za lami.

Miundombinu mingine ambayo Rais Dk. Samia amepania kuiboresha ni pamoja na viwanja vya ndege, bandari, meli, vivuko na madaraja katika maeneo mbalimbali nchini.

"Kazi anayopiga mama Samia inaonekana, si kazi ya mchezo, kila kona ukienda kuna barabara safi za lami na nyingine za changarawe, lakini katika kiwango kizuri kinachoruhusu barabara hizo kupitika bila matatizo hata wakati wa mvua. Mwenyezi Mungu, amjalie mama yetu," alisema Hizanti Chidye.

Hali kadhalika, Rais Samia amejikita katika utoaji wa huduma za kijamii zikiwemo elimu na afya kwa wananchi wa maeneo ya mijini na vijijini kwa kujenga zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, mikoa na rufaa.

Baadhi ya wachambuzi wa masuala ya kisiasa, wanasema katika kipindi hicho, Rais Dk. Samia ametekeleza kwa ufanisi mkubwa mipango mingi ya serikali anayoiongoza.

Wanasema hali hiyo imechangiwa kwa kiwango kikubwa na kuendelea kuimarika kwa usalama na utuvuli ndani na nje ya mipaka ya nchi, kunakowafanya wananchi kufanya shughuli zao kwa amani na utulivu mkubwa.

"Usalama na amani vinavyoendelea kuimarishwa na serikali yetu, ndiyo vitu vya muhimu sana katika utekelezaji wa haya yote tunayoongea leo kuhusu mambo makubwa yanayofanywa na mama yetu Rais wetu Dk. Samia. Nchi yetu imeendelea kuwa tulivu na kila mtu anafanya mambo yake kwa amani na kujiamini," alisema Rosada Kinjite, alipokuwa akizungumza na gazeti hili.

Rosada ambaye ni mmoja wa watu waliokuwa wakizungumzia miaka miwili ya Rais Samia kuwepo madarakani alisema mwanamke huyo wa shoka, amefanya mambo mengi ya kimaendeleo yanayostahili si tu kupongezwa, lakini pia yanayowavutia watu ndani na nje ya Tanzania. Amesema katika kipindi hicho kifupi, Rais ameliwezesha taifa kupiga hatua kubwa za kiuchumi kupitia uwekezaji mkubwa unaoendelea katika sekta za kilimo, madini, utalii na kadhalika.

Rosada aliyekuwa akizungumza kwa njia ya simu kutoka Mchomoro, Namtumbo, alisema kiongozi huyo wa nchi, ameonyesha dhamira na uzalendo wa kweli wa kuliwezesha taifa na wake kupiga hatua kubwa za kimaendeleo.

Katika uongozi wake, Rais Samia amekuwa akielekeza nguvu kubwa za serikali katika kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati na inayoleta matokeo chanya.

Inaendelea Uk.5

# Afisa Mtendaji wa Kata amfuta kazi mkandarasi

Na Abdul Mitumba, RUANGWA

AFISA Mtendaji wa Kata ya Nandagala wilayani Ruangwa katika Mkoa wa Lindi, Awesa Rashid, amemsimamisha kazi fundi aliyekuwa anajenga jengo la maabara katika Shule ya Sekondari Mary Majaliwa kwa tuhuma za kushindwa kukamilisha kazi kwa muda uliopangwa.

Mkandarasi huyo, Twahili Kawanga, amejikuta akipoteza kazi hiyo baada ya mkataba wake kwisha na hata alipoongezewa muda, pia alishindwa kukamilisha ujenzi na kukabidhi mradi huo wa vyumba viwili.

Kwa mujibu wa habari za uchunguzi ambazo Mwelekeo imezinasa, mkandarasi huyo alipokonywa rasmi kazi tangu Machi 8, mwaka huu baada kushindwa kukamilisha kazi na kukabidhi Januari 29, mwaka huu.

Kulingana na barua ya kumfuta kazi ya Afisa Mtendaji huyo kwenda kwa mkandarasi, imebainika kuwa Kawanga alishindwa kufanya kazi hiyo katika mazingira ya usafi na pia kushindwa kukamilisha kwa wakati.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya wiki tatu alizoongezewa ili kukamilisha kazi hiyo, lakini pia muda huo ukaisha bila kazi kukamilika.

"Baada ya kushindwa kukabidhi mradi, aliongezewa wiki tatu hadi 20, 2023, lakini pia alishindwa kukamilisha ujenzi na kukabidhi kazi hadi hatua ya kumpokonya mradi ikachukuliwa Machi 8, mwaka huu," ilisema sehemu ya barua hiyo.

Habari zinasema kuwa mradi huo umekataliwa na wahandisi wa Halmashauri na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo kutokana na kujengwa kinyume cha maelekezo ya viongozi na serikali.

Mkandarasi Kawanga alipozungumza na Mwelekeo kuhusua suala hilo, alikiri kupoteza kazi, akisema hatua hiyo imemsababishia kadhia kubwa, huku akisema hajui nini afanye ili awalipe mafundi wake wasaidizi ambao wanatoka nje ya Ruangwa.

"Gharama za ufundi kwenye ujenzi yote wa maabara hiyo ni Shilingi milioni 12 na hadi napokonywa deni lilibaki Sh.ilingi milioni 1.9 ukichanganya na fedha ambazo ningelipwa baada ya kupita muda wa matazamio imefika Shilingi 2.5, lakini kwa hatua iliyofikiwa kila kitu kimeharibika," alisema.

Kawanga alisema ameshindwa kumaliza ujenzi kwa wakati kutokana na kupata vifaa vichache na katika muda usiostahili na kwamba, kabla ya mradi huo alishajenga na kukamilisha kwa wakati miradi zaidi ya 50.

## Washauriwa kupeleka wasichana bweni

Na Mwandishi Wetu, Ruangwa

JAMII wilayani Ruangwa, imeshauriwa kuwapeleka wanafunzi wanafunzi wasichana bweni kama njia sahihi za kuwalinda wasikumbane na vishawishi vinavyowasababishia mimba za utotoni.

Hatua hiyo pia itasaidia kuwapa muda sahihi na wa kutosha watoto wa kike kujisomea na hatimaye kuwa katika nafasi nzuri ya kufaulu mitihani yao.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Ruangwa mkoani Lindi, Andrew Chikongwe, alipokuwa akizungumza katika hafla ya kuwakaribisha wanafunzi wa kidato cha kwanza katika Shule mpya ya Sekondati ya Marry Majaliwa.

Chikongwe ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Nandagala, alisema wazazi na walezi wanapaswa kuona umuhimu wa kuwapeleka watoto shule za bweni ili wapate wasaa wa kutosha wa kujisomea huku wakitunzwa vizuri. "Hatutaki na tukatae watoto wetu wa kike wakae nasi majumbani. Tuhamishie kwenye shule za bweni ambako ni salama hasa dhidi ya vijana wa mtaani ambao wanawapa changamoto nyingi mabinti zetu wanaokwenda na kurudi nyumbani kila siku," alisema.

Chikongwe alisema ili kuhamasisha wazazi na walezi kuwapeleka wasichana shule za bweni, atachangia Sh.15,000 kwa ajili ya kila mwanafunzi mwenye tatizo la godoro na kumuagiza Mkuu wa Shule kuwapokea wanafunzi wote hata kama wazazi wao hawajatimiza mahitaji ya chakula.

Alisema wazazi wa wanafunzi hao watapeleka kidogo kidogo fedha za mahitaji ya namna hiyo.

Mapema, mkuu wa shule hiyo, Alexander Frednand, alisema shule ina walimu 11 tu na wanne miongoni mwao ni wa kujitolea.

Marry Majaliwa Sekondari ni miongoni mwa shule mpya za Wilaya ya Ruangwa, ambayo ilianza rasmi kupokea wanafunzi Januari mwaka 2022 ikiwa na wanafunzi wa kidato cha kwanza na pili.

Kwa sasa ina jumla ya wanafunzi 178, kati yao wavulana 99 na wasichana 79 ambapo ni 78 pekee ndiyo wanaoishi bweni.

## Naura mbioni kurejesha huduma

Na Claud Gwandu, Arusha

BAADA ya kusitisha utoaji wa huduma kwa wateja kwa kipindi cha miaka mitano, Hoteli maarufu ya Naura Springs ya jijini Arusha huenda ikapata mwekezaji mpya hivi karibuni. Mwekezaji huyo atasaidia kufunguliwa kwa hoteli hiyo ya kitalii iliyoko katikati ya Jiji la Arusha. Tayari wawekezaji wenye majina makubwa katika uendeshaji wa hoteli za kitalii duniani, kutoka Uswisi, Falme za Kiarabu (UAE) na Afrika Kusini, wameonyesha nia ya kuwekeza katika hoteli hiyo iliyokuwa inaajiri zaidi ya wafanyakazi 200. Akizungumza mwishoni mwa wiki iliyopita kwa njia simu, Kaimu Mkurugenzi

Mtendaji wa Kundi la kampuni za Impala ambalo Naura Springs ni sehemu ya kundi hilo, Randle Mrema, alikiri kuwa wawekezaji hao wameonyesha nia ya kuweweza katika hoteli hiyo.

"Ni kweli, ni mapema mno kuwataja, lakini wawekezaji kadhaa wamejitokeza kutoka Uswisi, Falme za Kiarabu na hata Afrika Kusini na wanataka kuwekeza katika Hoteli ya Naura yenye hadhi ya nyota tatu, lakini tunachambua maombi yao.

"Bado ni mchakato wa ndani, lakini tutakapokamilisha umma utapewa taarifa," alisisitiza Mrema baada ya kundi hilo la mahoteli kutafuta mwekezaji katika matangazo yaliyotolewa hivi karibuni.

Hoteli nyingine maarufu jijini hapa zilizo chini ya kundi hilo ni pamoja na Impala yenyewe na Ngurdoto ambazo nazo hazitoi huduma kwa sababu mbalimbali.

Mrema alifafanua: "Tumepokea maombi yao na tunachambua tujue ofa ya kila mmoja ili tukubaliane namna bora ya kuendesha hii hoteli (Naura Springs). Kila kitu kinategemea masharti na makubaliano, lakini tuna matumaini kwamba mambo yataenda sawa."

Katika tangazo lililotoka mapema mwezi huu katika vyombo vya habari, menejimenti ya Kundi la kampuni za Impala Hoteli la Impala, iliwakaribisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi wenye uwezo wa kifedha na uzoefu wa kuendesha hoteli za kitalii kuwasilisha maombi ya kuendesha hoteli hiyo iliyo katika barabara ya Afrika Mashariki jijini hapa.

## `Bwawa la Nyerere, SGR viliniumiza akili'

Inatoka Uk.4

Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa barabara za lami na changarawe, zinazofungua kanda moja na nyingine, mkoa na mkoa na hata wilaya moja na nyingine.

Ujenzi wa miundombinu hiyo, unalenga kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji wa shehena za mizigo ikiwemo ya mazao ya kilimo kwenda kwenye masoko ya kuaminika na hivyo kuwawezesha wananchi kunufaika na shughuli za kilimo.

Kwa mujibu wa hotuba ya bajeti ya waziri mkuu katika mwaka wa fedha wa 2021/22, serikali imejenga jumla ya kilomita 251.9 za barabara kwa kiwango cha lami zilizohusisha barabara kuu, barabara za mikoa na wilaya. Lengo ni kuhakikisha kuwa makao makuu ya mikoa yote na nchi jirani zinaunganishwa kwa mtandao wa barabara za lami.

Miundombinu mingine ambayo Rais Samia amepania kuiboresha ni pamoja na viwanja vya ndege, bandari, meli, vivuko na madaraja katika maeneo mbalimbali nchini.

"Kazi anayopiga Mama Samia inaonekana, si kazi ya mchezo, kila kona ukienda kuna barabara safi za lami na nyingine za changarawe lakini katika kiwango kizuri kinachoruhusu barabara hizo kupitika bila matatizo hata wakati wa mvua. Mwenyezi Mungu, amjaalie mama yetu," alisema Hizanti Chidye.

Lakini pia Rais Samia amekuwa muumini mkubwa wa dhana ya kujenga uchumi imara kupitia sekta ya kilimo.

Hivi karibuni aliwahakikishia wadau wa maendeleo duniani kuwa Tanzania

itafanikisha ukuaji wa sekta ya kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030 ikilinganishwa na ukuaji wa sasa wa asilimia 3.6.

Alikuwa akizungumza katika Mkutano wa Jukwaa la Uchumi la Dunia (WEF) uliofanyika jijini Davos nchini Uswisi, ambapo aligusia namna sekta ya kilimo inavyotarajiwa kukua huku akibainisha mikakati

inavyoendelea kutekelezwa na serikali kupitia wizara ya kilimo.

Baadhi ya mambo ambayo Rais Samia aliyaainisha kama nguzo katika kuchochea ukuaji huo, kuwa ni pamoja na mageuzi yanayoendelea katika sekta ya kilimo hasa kuanzishwa kwa mpango wa vijana kujikita kwenye kilimo.

Hali kadhalika, kuongeza kiwango cha bajeti ya serikali katika sekta hiyo.

Katika mwaka huu wa fedha wa 2022/23 bajeti ya kilimo imeongezeka mara nne zaidi ikilinganishwa na mwaka 2021/22.

Ongezeko hilo limeifanya serikali kuwa na uwanja wa kuanza kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima, ruzuku ambayo itamwezesha mkulima kupata mbolea kwa bei nafuu hasa wakati huu ambako bei yake iko juu kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo vita vya Urusi na Ukraine.

Tangu enzi ya Rais wa Kwanza wa Tanzania, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kilimo kimekuwa kikitajwa kuwa ndiyo uti wa mgongo wa uchumi, dhana ambayo inazidi kuendelea kuaminiwa.

Hali kadhalika, Rais Samia amejikita katika utoaji wa huduma za kijamii zikiwemo za elimu, nishati na afya kwa wananchi wa maeneo yote ya mijini na vijijini kwa kujenga zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, mikoa na rufaa.

Hatua hiyo inayoambatana na upatikanaji wa dawa kwa unafuu katika vituo hivyo, inasaidia kuboresha afya za wananchi ikiwa ni pamoja na kuokoa maisha ya wanawake wajawazito na watoto wachanga.

"Ni jambo la kufurahisha kuona kinamama wajawazito sasa wanapata huduma katika vituo vya afya vilivyo karibu na maeneo wanayoishi tofauti na ilivyokuwa katika miaka ya nyuma ambapo wengi walisafiri umbali mrefu kufuata huduma. Tulishuhudia baadhi yao wakipoteza maisha wao na watoto wakiwa njiani kupelekwa hospitali," alinena mkazi mmoja wa Vianza wilayani Mkuranga.

Hata hivyo, mwananchi huyo, hakutaka jina lake litajwe lakini alisema hatua hiyo inadhihirisha dhamira ya kweli ya Rais Samia ya kuhakikisha kuwa huduma za afya, zinawafikia wananchi kwa urahisi.

Katika kipindi cha mwaka huu wa fedha, Rais Samia ameridhia Sh. bilioni 160 zitumike kugharimia ujenzi wa vyumba 8,000 vya madarasa katika shule za msingi na sekondari kote nchini.

Ujenzi wa vyumba hivyo unalenga katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaostahili kwenda shule, wanapata nafasi huku kukiwa na uhakika wa kuondokana na tatizo la kusoma kwa zamu.

Vyumba hivyo vimejengwa sambamba na samani zake.

Pamoja na mafanikio hayo, kwa sasa serikali inakabiliwa na changamoto ya mfumuko wa bei unaozikabili pia serikali za nchi nyingine duniani.

Hali hiyo ilitokana na kuzuka kwa ugonjwa wa UVIKO-19 na vita vinavyoendelea kati ya Urusi na Ukraine, vimesababisha makali ya maisha miongoni mwa wananchi na kuitaka serikali ichukue hatua.

Wananchi hao wanadai kuwa mfumko wa bei umesababisha kupanda kwa bei za bidhaa na hasa vyakula wakati upatikanaji wa fedha ukiwa mgumu.

Serikali iliwahi kukiri kuhusu kuwepo kwa tatizo la mfumuko wa bei na kwamba kunachangiwa na kuvurugika kwa mnyororo wa uzalishaji wa bidhaa duniani.


# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO



### Wanafunzi na vijana kutowapisha wazee `siti' ndani ya mwendokasi

**Utamkuta kikongwe, mjamzito, mwenye ulemavu, wamesimama ndani ya mwendokasi huku vijana na wanafunzi wakiwa wamejaa tele kwenye viti! Vijana hao wakishakaa kwenye siti, huinamisha vichwa vyao chini wakijifanya ama wamelala, wanachat na simu zao janja au wamenogewa na mziki wanaousikiliza wakiwa wamebandika `vinasa sauti' (ear phones) masikioni mwao. Mbaya zaidi hata baadhi ya wazazi hudiriki kukaa na watoto wao kila mmoja katika siti yake huku wakijifaya hawawaoni watu hao wenye mahitaji maalum. Tubadilike na kuisadia jamii yenye mahitaji maalum.**




MAONI YA MHARIRI

## MaDC zingatieni maagizo ya Dk. Mpango

JUZI, Makamu wa Rais, Dk. Philipo Mpango, alitoa maagizo mazito kwa wakuu wa wilaya alipokuwa akifungua mafunzo ya uongozi kwa viongozi hao jijini Dodoma.

Pamoja na mambo mengine, Makamu wa Rais aliwataka wakuu wa wilaya kuzingatia utawala bora, kanuni, sheria, utaratibu katika uongozi na utatuzi wa migogoro katika maeneo yao.

Alisema ni vema viongozi hao kuzingatia maadili ikiwemo kudhibiti uvujaji wa siri za serikali kwa kujiepusha na matumizi yasiofaa ya mitandao ya kijamii pamoja na barua pepe binafsi katika kutuma nyaraka za serikali.

Kadhalika, alitoa wito kwa wakuu wa wilaya kuzingatia utaratibu katika matumizi ya walinzi binafsi na waandishi wa habari katika ofisi za umma.

Mbali na hayo, aliwataka kuwa wepesi na wabunifu katika kutatua migogoro hususan ya ardhi na mipaka, migogoro baina ya wakulima na wafugaji na baina ya wafugaji au wakulima na hifadhi na kuhakikisha hakuna migogoro mipya inayoibuka katika maeneo yao.

Vile vile, aliwahimiza kuhakikisha kwamba wanadhibiti uhasama ndani ya jamii au na vyombo vya dola, mauaji na kuwa walinzi wa haki za watu wote hususani wanawake na watoto.

Lakini pia, aliwataka wakuu hao wa wilaya, kusimamia miradi inayotekelezwa katika maeneo yao kwa kuhakikisha inakamilika kwa wakati na viwango vilivyokusudiwa.


Kimsingi, maagizo haya na mengine mengi aliyotoa Makamu wa Rais,.yanapaswa kuzingatiwa si katika kusimamia utawala bora, lakini pia maendeleo ya kiuchumi ya Taifa.

Wakuu wa wilaya ambao ni wawakilishi wa Rais katika maeneo yao, ni viongozi muhimu wanaopaswa kuwa karibu na wananchi kutatua matatizo yao, lakini wakiwa ndiyo watunzaji wakubwa wa siri za serikali.

Mwelekeo tunaunga mkono maagizo haya ya Dk. Mpango tunachowasihi wakuu wa wilaya zote nchini, kuyazingatia na kuyatekeleza kwa umakini mkubwa.

UMGL MEDIA Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255693257410 / 0766005061
**Mhariri Michezo:** +255713055011 / 0621350860
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** jaridalamwekeleo@gmail.com



Na Prosper Mhadisa
JICHO LANGU
jaridamwelekeo@gmail.com

## Kuna umuhimu wa kujali muda

SIKU zote mafanikio ya mtu yanatokana na nguvu anayoitumia katika kutekeleza jambo analolifanya kwa faida yake au hata jamii.

Hata hivyo, suala la muda lazima lipewe kipaumbele katika utendaji wa jambo hilo.

Lakini, kwetu sisi wa eneo la ukanda wa Afrika Mashariki, suala la muda wala si la msingi sana yaani halipewi msukumo mkubwa katika utendaji wa jambo fulani liwe la mtu binafsi au la jamii.

Jambo hili linasababisha jamii yetu ionekane kuwa ni ya watu wavivu na wasiokuwa na matamanio ya kimaendeleo.

Ni kweli kwamba majukumu yetu ni mengi sana, lakini kuna haja ya kuyapangilia ili tuyafanye kwa wakati na hivyo kufikia maendeleo.

Utendaji wa mambo kwa wakati, unamfanya mtendaji au watendaji, kujiamini na hatimaye kuepuka kutegemea msaada wa wengine.

Mtu anayeweza kuutumia vizuri muda wake, kwa namna yoyote, atakuwa na utaratibu mzuri wa mambo yake na wala hawezi kuwa kero kwa watu wa aina yake.

Mara nyingi tunapozungukwa na watu wengine tukiwa hatuzingatii suala la muda, tunakuwa na hofu ya kufanya uamuzi kwa ufasaha.

Jambo la muhimu hapa ni kuwa, jaribu kutenga muda mzuri wa kutosha kufikiria kazi yako na mambo yako ya msingi huku ukiwa peke yako.

Kufanya hivyo, kutakusaidia kufanya uamuzi kuhusu kutekeleza majukumu yako na hatimaye kufikia uamuzi

> **Mara nyingi tunapozungukwa na watu wengine tukiwa hatuzingatii suala la muda, tunakuwa na hofu ya kufanya uamuzi kwa ufasaha....**

Muda husaidia pia katika kusafisha akili. Mara nyingi akili zetu zinajazwa na taarifa kutoka kwenye kazi, mitandao, marafiki na hata familia.

Ikiwa mtu atatenga muda vizuri na kuujali, basi itamsaidia kuondokana na akili ya namna hiyo na kuwa sawa kimawazo.

Wakati mwingine, matumizi mazuri ya muda hutatua changamoto mbalimbali.

Njia bora ya kutatua matatizo inakuja pale ambapo unakuwa na uhuru wa kuwa peke yako.

Kutumia muda vizuri ukiwa peke yako kutakusaidia kuwa na uwezo wa kufikiria matatizo na njia sahihi za kutatua matatizo.

Kuwa peke yako inarahisisha uwezo wa kufikiria chanzo cha tatizo na njia tofauti za kushughulikia.

# Miaka miwili ya Samia Suluhu Hassan, yachochea kukua kwa kasi kwa sekta ya nyumba

## NHC yaongeza kasi ya ujenzi wa nyumba, kuhuisha sera ya ubia

**Na Mwandishi Wetu**

MIAKA miwili ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ameikwamua miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), iliyokuwa imesimama ya Morocco Square, Kawe 711 Plot 300 Regent Estate. Miradi hiyo imeendelea kutekelezwa baada ya NHC kupata mkopo wa Sh. Bilioni 44.7 kutoka Benki ya CRDB na NMB ambazo zimetumika kumalizia ujenzi wa Mradi wa Morocco Square (Sh. bilioni 25.7) na Sh. Bilioni 19 zilitengwa kwa ajili ya mradi wa Plot 300 Regent Estate Dar es Salaam.

Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango, Februari 2023 iliruhusu Shirika kupewa fedha za mikopo kukamilisha miradi mingine iliyosimama ikiwemo Kawe 711 na mradi mpya ujulikanao kwa jina la Samia Housing Scheme (SHS), wa nyumba za watu wa kipato cha chini na cha kati ambao umeanza kutekelezwa jijini Dar es Salaam.

### KUONGEZA KASI YA UJENZI

Katika kipindi cha uongozi wa miaka miwili, Serikali ya awamu ya sita ililipatia Shirika mkopo nafuu wa Sh. bilioni 20 ili kuongeza kasi ya ujenzi wa nyumba 1,000 jijini Dodoma. Fedha hizo zimewezesha ujenzi wa nyumba 404 na Shirika limenunua ardhi maeneo ya Njedengwa ili kuwezesha ujenzi wa nyumba hizo.

Aidha, kutokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais kumesaidia NHC kutekeleza mradi SHS utakaowezesha ujenzi wa nyumba 5,000 nchini zitakazogharimu Sh. bilioni 466.

Kwa sasa NHC limeanza ujenzi huo katika eneo la Kawe jijini Dar es Salaam ambapo nyumba 560 zimeanza kujengwa.

### SAMIA AIPATIA NHC MIRADI YA UKANDARASI

Rais Dk. Samia alilipatia Shirika la Nyumba la Taifa miradi mikubwa minane ya Wizara za Serikali inayogharimu Sh. bilioni 106 iliyoko jijini Dodoma. Miradi hii ya Wizara nane za Serikali inatarajiwa kukamilika kati ya Oktoba hadi Desemba 2023. Wizara zinazohusika ni Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Nishati, Madini, Habari na Mawasiliano, Mifugo na Uvuvi, Viwanda na Biashara, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Mambo ya Ndani.

Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita imelipatia Shirika miradi ya ukandarasi wa ujenzi wa Ofisi za Wakala wa Ununuzi na Ugavi Serikalini (GIPSA), yenye thamani ya Sh. 2.8 bilioni. Miradi hii inajengwa Kibaha, Mtumba-Dodoma, Simiyu na Songwe.

Vilevile, Serikali hii imelipatia Shirika kufanya kazi ya ujenzi wa majengo mengine katika Hospitali ya Ligula mkoani Mtwara. Ujenzi huo ulianza Aprili 2022 na utakamilika Juni 2023 kwa gharama ya shilini billion 2.7.

### KUWEZESHA SERA YA UBIA

Katika kipindi cha miaka miwili, sekta ya nyumba imeendelea kupata maelekezo kutoka Serikali ya awamu ya sita kuendelea kuchochea mashirikiano kati ya sekta binafsi na sekta ya umma, kwa lengo la kuboresha upatinaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na kuunda Idara kamili ya nyumba kwenye Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya makazi. Hali kadhalika sasa Serikali imehakikisha inasimamia kuwapo kwa sera ya nyumba ambayo ndiyo muongozo muhimu kwa sekta hii ya nyumba nchini.

Shirika la Nyumba la Taifa Kutokana na msukumo wa Serika;li ya awamu ya sita juu ya kufungua uchumi wa nchi na kushirikisha sekta binafsi kama injini ya maendeleo endelevu,lilipokea maelekezo ya

Mheshimiwa Rais kwa kupitia upya na kuiboresha sera ya ubia ambayo ilizinduliwa rasmi na Waziri Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Kasim Majaliwa Majaliwa Novemba 16, 2022 jijini Dar es Salaam.

Ni katika muktadha huu tumeshuhudia kufumuka kwa ujenzi wa nyumba katika maeneo mbalimbali nchini, kichocheo kikubwa kikiwa ni sera ya ubia kama ilivyofanyiwa kazi na shirika ambako kumeimarisha uchumi wa mtu mmoja mmoja na wa Taifa kwa ujumla.

Serikali ya awamu ya sita ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan inatimiza miaka miwili huku ikiwa imeelekeza nguvu kubwa katika kuinua uchumi wa Tanzania na maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

Juhudi hizo zinazolenga kuleta ustawi kwa Watanzania na nchi kwa ujumla na kutoa ajira, kukuza mapato ya serikali, kukuza sekta ya fedha kupitia mikopo ya nyumba watengenezaji, wauzaji na wakandarasi kukopa kwa ajili ya kutekeleza majukumu.

Pia kukuza soko la sekta za huduma kama umeme, maji, gesi, simu, habari (matangazo), ulinzi, kuongeza maisha bora kwa wananchi na kuwa na mandhari nzuri na miji iliyopangwa. Hata hivyo, bado kuna changamoto kubwa katika kufikia lengo hilo kwani asilimia 70 ya miji yetu haijapimwa.

Sera bora za sekta zote zikifanyiwa maboresho yanayoendana na mahitaji ya soko, kama zilivyo sekta zingine sekta ya nyumba na makazi ni sekta mtambuka yenye mchango mahususi na ni kichocheo kikubwa katika uchumi wa taifa kwani itazalisha ajira nyingi na kujenga uchumi mkubwa wa nchi.Mnyumbuliko wa sera bora katika sekta nyingi za maendeleo ikiwemo sekta ya nyumba na makazi kunachochea kukua kwa pato la taifa ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa sekta mbalimbali hususani barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii, huduma za maji, utawala bora, mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi, pamoja na kuhamasisha uwekezaji kuna athari kubwa na chanya kwenye maendeleo ya sekta ya nyumba na makazi nchini.

Serikali ya Dk. Samia imehakikisha sera za mapato na matumizi zinajikita katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa. Msukumo mkubwa umejikita katika kuhakikisha usimamizi madhubuti wa fedha za umma na kuzielekeza kwenye maeneo yatakayoongeza tija, ajira na kuinua uchumi wa mwananchi mmoja mmoja.

Serikali ya Awamu ya Sita imetuhakikishia kwamba miradi ya kipaumbele na kimkakati inayoendelea kutekelezwa inakamilika kwa wakati ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi mipya.

NHC ambalo ndilo kiongozi wa uendelezaji wa miliki, katika awamu hii ya sita ujenzi wa nyumba umechanua, uchumi wa Shirika umeongezeka na Shirika limeendelea kufanya majukumu yake ya ujenzi wa nyumba za makazi na biashara kwa ajili ya kuuza na kupangisha.

Majukumu ya Shirika yanatekelezwa kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa Shirika wa Miaka 10 (2015/16 – 2024/25) ambao unalenga kusukuma mbele ujenzi wa nyumba zipatazo 10,000 na kuwezesha ukuaji wa sekta ya nyumba kupitia ushirikishwaji wa sekta binafsi.

Shirika la Nyumba lina mtaji (capital base) wa Shilingi trilioni 5.04 hivi sasa unaotokana na rasilimali ya majengo yake 2,650 yenye nyumba(Units) zipatazo 18,654 zilizopo katika mikoa mbalimbali nchini.

Haya ni miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa awamu ya sita kama inavyoainishwa katika makala haya.




**Morocco Square: Muonekano wa majengo ya Morocco Square katika picha zilizojengwa na kukamilika kwenye eneo la Morocco jijini Dar es Salaam.**




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, akishuhudia uwekaji saini makubaliano ya awali ya mkataba wa nchi hodhi (HGA) wa mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia kuwa kimininika (LNG) katika hafla iliyofanyika Juni, mwaka jana Ikulu Chamwino jijijini Dodoma. (PICHA: TPDC)

# TPDC na uwekezaji mkubwa miaka miwili ya Dk. Samia

**Na Mwandishi Wetu**

MIAKA miwili ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan madarakani, imetajwa kugusa gesi asilia kwa namna ya pekee huku ikishuhudiwa uwekezaji mkubwa katika eneo hilo ambao utagharimu mabilioni ya fedha.

Taarifa ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), kwa gazeti hili jana inaeleza kuwa katika kipindi cha miaka miwili ya Awamu ya Sita, Serikali imefanikisha uwekaji saini wa makubaliano ya awali ya mkataba baina ya Tanzania na kampuni nane zilizogundua gesi.

Inaeleza kuwa mkataba huo uliosainiwa Juni, mwaka jana mbele ya Rais Samia, ulikuwa wa vitalu namba 1, 2 na 4 vilivyopo katika kina cha bahari ya Hindi.

Inaeleza kuwa utiaji saini huo unaweka msingi wa kukamilisha majadiliano ya mkataba wa 'Host Government Agreement' na mikataba mingine ya utekelezaji wa mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia.

"Uwekezaji katika mradi huu unatarajiwa kugharimu takriban Sh. trilioni 70 za kitanzania ambapo kwa mujibu watafiti, takribani asilimia 10 ya kiasi hiki kitatumika ndani ya nchi katika kipindi ambacho mradi upo katika hatua za ujenzi," taarifa ya TPDC inakariri maneno ya Rais Samia aliyoyazungumza wakati wa hafla ya uwekaji saini mikataba hiyo.

Inaeleza kuwa fedha hizo zinatarajiwa kutumika katika ununuzi wa vifaa na huduma hapa nchini ikiwemo usafirishaji, ukodishaji wa mitambo, mafuta ya dizeli na vilainishi, chakula, ulinzi, huduma za kifedha, huduma za afya, bima na malazi.

Taarifa hiyo inafafanua kuwa utekelezaji wa mradi huo katika Mkoa wa Lindi utafanyika sambamba na uendelezaji wa miundombinu kwenye mkondo wa juu ili kuwezesha kuvuna rasilimali hiyo.

Inasema serikali ya awamu ya sita imeweka mazingira wezeshi kwa Watanzania hususan wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara, kunufaika na gesi asilia pamoja na miradi mingine ya kimkakati.

"Mradi huu ni wa nchi nzima, lakini kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara lazima wayaone manufaa ya mradi huu, hivyo tusisahau mazingira mahususi ya mikoa hii wakati wa majadiliano. Mchakato wa majadiliano, maandalizi na utekelezaji wa mradi lazima yapelekee kujenga uwezo wa Watanzania kwenye sekta hii, dhamira yetu ni kwamba katika miaka ijayo, vizazi vijavyo viweze kuvuna rasilimali za nchi kwa tija zaidi, manufaa zaidi na kwa kujitegemea zaidi," anakaririwa Dk. Samia katika taarifa hiyo.

Inaelezwa kwamba utekelezaji wa mradi wa LNG utachochea ukuaji wa uchumi, kuiongezea serikali mapato, kuongeza ajira na kuongeza uwezo wa Watanzania kitaaluma.

Wakati wa kusaini makubaliano hayo, Waziri wa Nishati, January Makamba, anakaririwa akieleza kuwa mradi huo kuzalisha ajira 10,000 katika kipindi cha miaka minne hadi sita.

**Tunatambua jitihada za serikali ya Awamu ya Sita kwa kuweka kipaumbele katika mradi huu...**



Aidha, anasema baada ya kukamilika, ajira za kudumu zitakazopatikana ni 500 na kwamba wizara yake imejipanga kuhakikisha Watanzania wanashiriki kwa ufanisi na kupata uzoefu.

TPDC katika taarifa yake linaeleza kuwa kampuni za mafuta za kimataifa zinazotekeleza mradi huo kwa kushirkiana na Serikali zinatambua juhudi za nchi katika kuwezesha sekta ya mafuta na gesi.

"Tunatambua jitihada za serikali ya Awamu ya Sita kwa kuweka kipaumbele katika mradi huu, tunashukuru kwa nafasi mliyotupa ya kufanyakazi na Waziri Makamba pamoja na viongozi wengine wa Serikali," anasema Jared Kuehi, Makamu wa Rais na Meneja Mkazi wa Kampuni ya Shell pamoja na Unni Fjaer, Meneja Mkazi wa Kampuni ya Equinor.

Mwaka 2010 hadi 2016, Serikali kwa kushirikiana na kampuni tano za mafuta za kimataifa zilihusika katika ugunduzi wa gesi asilia hapa nchini.

Takwimu zinaonesha kwamba hadi kufikia Februari 2023, jumla ya futi za ujazo trilioni 57.54 za gesi asilia zimegunduliwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, jumla ya futi za ujazo trilioni 47.13 zipo katika vitalu vilivyopo katika kina kirefu cha

Bahari ya Hindi na futi za ujazo trilioni 10.41 zipo katika maeneo ya nchi kavu.

Kufuatia ugunduzi huo, Serikali ilifanya maamuzi ya kuendeleza gesi hiyo kwa kuibadili kutoka katika hali ya hewa na kwenda katika hali yakimiminika. (Liquefied Natural Gas - gesi asilia iliyiochakatwa na kuwekwa katika hali ya kimiminika LNG), ili iweze kutumika kwa matumizi mbalimbali ndani ya nchi na pia kuwezesha usafirishaji wake kwa wingi kwenda katika masoko ya kimataifa. Mradi wa LNG ni moja ya miradi ya kimkakati inayotekelezwa na TPDC chini ya Wizara ya Nishati.

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Mweleko

JARIDA

# Jungu kuu

Jumatano Machi, 15-21, 2023




**Jarida hili haliuzwi**



# Rais Dk. Samia anavyogusa mioyo ya wanawake




UK. 11

**'Ushoga na dhana ya kuoana jinsia moja. Je; ni halali?**

**Je; wajua athari za kuangalia runinga kwa muda mrefu?**



UK. 16

Jamii

Na Dk. Felician Kilahama

# 'Ushoga na dhana ya kuoana jinsia moja. Je; ni halali? - 2

KATIKA sehemu ya kwanza ya makala hii, nilihitimisha kwa maelezo kwamba 'Hawa' alitwaliwa katika mwanaume, hivyo mwanaume atawaacha wazazi wake (baba na mama); naye ataambatana na mwanamke na hao wawili watakuwa 'mwili mmoja.'

Sasa taswira za 'mwanaume kumuoa 'mwanamme' (gays) au 'mwanamke' kuolewa/kuoa 'mwanamke' (lesbian), zinatoka wapi?

Kusema kweli hali hiyo ni 'kukengeuka' na kuvunja 'misingi ya ndoa' kama ilivyowekwa na Mungu kuhusu kuishi mume na mke.

Utaratibu huu wa mume kumuoa mume mwenzake au mwanamke kumuoa mwanamke mwenzake, ni ushetani uliopitiliza na haukubaliki hata kidogo.

Kumbuka tunaonywa kwamba tutaangamizwa kwa kukosa maarifa, shetani amejizatiti kuwaangamiza baadhi ya binadamu kwa kutumia 'dhana ya kupendana' eti ni haki ya msingi kwa 'mashoga' kufanya hivyo wakati ni 'uovu' wa aina yake.

Binadamu, unamtamani mume mwenzako au mwanamke unamtamani mwanamke mwenzako? Ili iweje? Eti kuishi pamoja kama wanandoa wengine (mume na mke), hii ni hatari sana maana hata wanyama wa porini hawako hivyo.

Najiuliza, watu wenye tabia hizo wananufaika na nini katika huo 'upendo' kinyume cha mapenzi ya Mungu? Kuna faida gani kwa binadamu aliyeumbwa kwa mfano na sura yake Mungu kufanya uovu kama huo?

Kwa bahati mbaya sana, kuna watu wengine ambao si mashoga, lakini wanaupigia debe 'ushoga', kwa kusema hadharani kuwa 'mashoga' ni binadamu na kwamba kama wanadamu wengine, wanahitaji faragha.

Sawa, wao ni binadamu hatukatai, lakini wamekengeuka misingi ya ubinadamu.

Haiwezekani katika hali ya kawaida mwanamume abadilishe jinsia yake ya kiume na kuwa mwanamke, hali kadhalika na mwanamke.

Hali hiyo haimpendezi Mwenyezi Mungu aliyetuumba. Huo ndiyo ukweli na siyo kinyume chake.

Hata kama wataalam wakifanya mabadiliko na kukuwekea watu hao jinsia za kike, bado watabaki kuwa wanamume tu.

Imeeandikwa mwanaume atawaacha wazazi wake (baba na mama) ataambatana na mwanamke na hao wawili watakuwa mwili mmoja'. Hakuna iliposajiliwa kwamba 'mwanaume atawaacha wazazi wake: ataambatana na mwanamume mwenzake na kuwa mwili mmoja'.

Vivyo hivyo kwa mwanamke na mwanamke. 'Ushoga' kwa




maana ya watu wa jinsia moja kuwa 'mume' na 'mke' ni kwenda kinyume cha kusudio la Mwenyezi Mungu aliyeumba jinsia mbili tofauti; ili hawa wawili wakikaa pamoja kama 'mume' na 'mke', binadamu wataongezeka na kuijaza nchi.

Kimsingi, 'ushoga' hauna maana yoyote isipokuwa ni 'roho/nafsi' zenye kuzingirwa na 'uovu' chini ya 'wakuu wa anga na wafalme wa giza katika ulimwengu wa roho.'

Hii ndiyo 'vita ya kiroho' tunayotakiwa kupigana nayo hadi ushindi upatikane. Hapa tunahitaji nguvu ya Neno la Mungu pamoja na kutii na kunyenyekea ili yeye anayefahamu yaliyomo ndani ya nafsi au roho zetu, atuepushe na mambo kama haya yasiyokuwa na 'mbele wala nyuma' maana ni 'giza tupu'.

Mungu alituumba binadamu ili tumpe Utukufu na heshima anayostahili na si kufanya mambo ya ovyo wakati alituumba kwa mfano na sura yake. Ushoga' ni aibu kubwa kwetu. Kwa bahati mbaya mataifa yaliyoendelea sana ndiyo chimbuko la 'aibu' hii kwa binadamu.

Kuendelea kwao ndiyo msingi wa haya yote ikiwemo kumuweka Mungu kando wakidhani kuwa na kila kitu ni ruhusa kwa watu kufanya wanavyotaka hata kama ni kinyume cha mapenzi yake Mungu.

Kutokana na mtazamo huo, hawajali mtu anafanya uovu gani hivyo wakafika mahali 'ushoga' ukapewa hadhi sawa na waliooana wa jinsia tofauti. Utawala unaweka Sera na Sheria zinazohalalisha 'ushoga'. Kadhalika, imetengenezwa bendera ya 'ushoga' ambayo rangi zake zinashabihiana na rangi za 'upinde wa mvua'.

Hatari zaidi ni kuona hata baadhi ya madhehebu ya dini katika mataifa hayo, kushabikia na kuunga mkono 'ushoga'.

Unakaa na kujiuliza kwamba hivi madhehebu hayo yanafanya hivyo ili iweje? Hakika matendo haya ni 'kukufuru' kwa sababu yanakwenda kinyume cha maadili ya kiroho.

Hata vijana wetu wengi wamejikuta wemeingia katika mkumbo huo kwa kutazama na kuiga masuala yasiyofaa yanayovyofanyika katika mataifa mengine; tabia ambazo ni kinyume na maadili yetu.

Mfano, wanaovaa suruali/kaptura 'milegezo' maanake nini? Ni dalili zisizofaa za 'kiushoga ushoga.'

Hali kadhalika, msichana au mwanamke kuvaa 'kisuruali' kinachobana na kuonyesha maumbile yake kimwili, hizo ni dalili za uovu tu.

Baadhi yetu, tunashabikia na kutetea mambo haya kwa hoja kwamba ni 'haki za binadamu' wakati tukijua kuwa siyo sahihi maana ni kinyume cha maadili na tabia njema.

Haki gani hizo 'wanaume' au 'wanawake' kujifanya 'mume na mke' ni kukengeuka kwa hali ya juu katika historia ya binadamu.

> **Ipo 'hoja' kuwa binadamu wote tumekosa mbele za Mungu hivyo wote tunatenda dhambi na hakuna aliye msafi mbele za Mola...**

Niwaombe viongozi wetu wa kiroho (madhehebu mbalimbali), wasimame imara kupinga jambo hili lenye ukakasi mkubwa kuingizwa katika masuala ya kiroho.

Kadhalika, inashangaza kupindukia unapomwona aliyewekwa 'wakfu' na 'mchunga kondoo wa Mungu' anageuka kuwa 'shoga' na kuendelea kutoa huduma kwa waumini wa madhehebu yake?

Je, kama kuna taratibu za wahusika kufunga ndoa, inakuwaje mfano, masuala ya 'mahari', Sheria za kufanya hivyo? Kama sikosei Sheria ya Ndoa Tanzania imejengeka kwenye msingi wa mwanamume kuachana na wazazi wake na kuandamana na mwanamke, hivyo wakafunga ndoa na kuanzisha familia 'mpya' kama sehemu ya jamii.

Matakwa haya ya msingi hayaendani kabisa na 'ndoa' za 'kishoga' maana ni kuanzisha familia 'feki.

Ipo 'hoja' kuwa binadamu wote tumekosa mbele za Mungu hivyo wote tunatenda dhambi na hakuna aliye msafi mbele za Mola. Sawa, lakini kisiwe kigezo cha watu wa jinsia moja kujifanya 'mume' na 'mke' kinyume cha maumbile.

Kuhalalisha uovu katika jamii, ni hatari sana sijui ni dhambi ya 'uzinifu/uasherati' maana haiingii akilini kusema wenye jinsia moja wamefanya dhambi hiyo, lakini kwa mtazamo wa 'uongo' maana kujifanya 'mume'/'mke' wakati kimaumbile mhusika hayuko hivyo, ni uongo.

Naomba viongozi wa serikali (ngazi zote) na wale wa kisiasa nchini, wasimame kidete ili jambo hili lisipate nafasi ya kuhalalishwa kisera wala kisheria ili kulinda maadili ya taifa letu.

Viongozi wetu wakemee 'ushoga' kwa nguvu zote na kwa moyo wa upole, wahusika washauriwe ili waachane na tabia hiyo mbaya na ovu kupindukia.

Tusihalalishe 'uovu juu ya uovu' kwa kisingizio kuwa hakuna aliye msafi isipokuwa Mungu mwenyewe.

Waliozaliwa wakiwa wanaume, wabaki kuwa wanaume na waliozaliwa wakiwa wanawake, wabaki kuwa wanawake na tuendeleze vizazi kupitia taasisi ya ndoa na siyo kinyume chake.

Ni Mungu mwenyewe aliyeanzisha taasisi hii na kwa hiyo lazima iheshimiwe sana na kila mtu. Kinyume cha hapo 'ushoga,' ni kuikosesha heshima 'ndoa' halali, inayostahili sawa sawa na makusudi ya muumba wetu.

**Mungu ibariki Tanzanua, Mungu ibariki Afrika.**

## Jamii

# Je; wajua Tanangozi, Iringa imetokana na nini?

## Ni kweli watu wanakula nyama ya mbwa?

**Na Mwandishi Wetu**

KAMA ukiwauliza wahenga na wenyeji wa Kijiji cha Tanangozi kuhusu asili ya jina la kijiji chao, watakueleza kuwa kimsingi, jina halisi ni `Tana vagosi' na siyo Tanangozi, kwa Kiswahili ikimaanisha kuwa `wanaume wamegoma/kataa kutoka.'

Imeelezwa kwamba, awali eneo hilo la Tanangozi, lilikuwa ni kambi la askari wa Chifu Mkwawa. Askari hao wanadaiwa kuwa ni wale waliokuwa wakakamavu, shupavu na wasio waoga kumkabili adui ambao kwa mfumo wa majeshi ya sasa, wanaitwa makomandoo.

Wanasema jina la Tanangozi lilitokana na wazungu/wakoloni kushindwa kutamka neno la Kihehe la Tana vagosi.

Wanasema jina hilo la Tana vagosi, yaani wanaume wamegoma kutoka, lilikuja wakati wa vita vya makabila kati ya Wahehe na Wangoni.

Inasemekana wakati wa vita vya Wahehe na Wangoni kutoka mkoani Ruvuma ambao ni watani wakubwa wa Wahehe, vilipofika eneo la Tanangozi, askari hao shupavu wa Mkwawa, waliweka msimamo kwamba, hapo sasa piga ua, hakuna mwanaume atakayetoka au kukimbia yaani Tana vagosi na ndipo lilipozaliwa rasmi jina la Tanangozi.

**Siri ya kudaiwa kuongoza kula nyama ya mbwa**

Historia ya madai hayo, inaweza kuanzia miaka ya 1968 baada ya kundi la wahitimu wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Tanangozi, iliyopo mita kadhaa kutoka Barabara Kuu ya Tanzania – Zambia.

Mara baada ya wanafunzi hao kuhitimu elimu yao na kukosa nafasi ya kuendelea na kidato cha kwanza kwa sababu ya uhaba wa shule za sekondari wakati huo, walibuni mbinu ya kujiajiri ili waendelee kupambana na maisha badala ya kuwategemea wazazi wao.

Ikumbukwe kuwa wakati huo, maeneo mengi hayakuwa na huduma za umeme na Kijiji cha Tanangozi kilikuwa miongoni mwa maeneo ya aina hiyo.

Kwa sababu hizo, wahitimu hao wa darasa la saba, walilazimika kubuni biashara zisizohitaji matumizi ya teknolojia ya umeme na kwa hiyo walibuni mradi wa kupika maandazi huku wengine wakichoma mishikaki ya nyama ya ng'ombe na kuuza katika kituo cha mabasi na malori yalikokuwa yakisafirisha mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Zambia na kutoka Zambia yakisafirisha shaba kuleta katika Bandari ya Dar es Salaam.

Nakumbuka mmoja wa wahitimu hao aliyeanzisha biashara ya kuuza maandazi, alikuwa William Asilia Masilu (marehemu na Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake mahali pema peponi).



**Kwa hiyo, kadiri miaka ilivyozidi kusogea na wahitimu wa darasa la saba wakiongezeka katika Kijiji cha Tanangozi, ndivyo biashara ya kuuza mishikaki ilivyozidi kushamiri...**

Hata hivyo, kwa bahati mbaya simkumbuki vizuri mwanzilishi wa kuchoma mishikaki na kuanza kuuza pale stendi ya Tanangozi, lakini alikuwa miongoni mwa wahitimu hao wa darasa la saba wa mwaka 1968.

Biashara iliyovuma kwa kasi zaidi na kuchangamkiwa na wahitimu wengi, ni hiyo ya kuuza mishikaki. Ilikuwa kila basi lililosimama kuteremsha ama kupakia abiria, wauzaji mishikaki walilikimbilia na kusimama madirishani na kuwauzia abiria mishikaki.

"Mishikaki! mishikaki! Ilikuwa ndiyo lugha iliyotumika na wauzaji hao wa mishikaki, kutangaza biashara yao huku wakiipitisha madirishani kiasi cha kuhatarisha `kuwatoboa' macho abiria waliokuwa wameyafungua.

Hali hiyo iliwafanya baadhi ya abiria wanapofika katika Kituo cha Mabasi cha Tanangozi, kulazimika kufunga madirisha kwa lengo la kukwepa kutobolewa macho na vijiti vya kuchomea mishikaki.

Kwa hiyo, kadiri miaka ilivyozidi kusogea na wahitimu wa darasa la saba wakiongezeka katika Kijiji cha Tanangozi, ndivyo biashara ya kuuza mishikaki ilivyozidi kushamiri.

Kwa msingi huo, eneo la Tanangozi likazidi kupata umaarufu wa uuzaji wa mishikaki na hali hiyo imeendelea hadi kufikia sasa.

Hata hivyo, baadhi ya watu hasa wa kutoka nje ya Mkoa wa Iringa, wakaanza kuitilia shaka mishikaki inayouzwa hapo wakidai kuwa si ya nyama ya ng'ombe bali ni ya nyama ya mbwa!

Uvumi huo uliendelea kusambaa ndani na nje ya Mkoa wa Iringa na hadi sasa baadhi ya watu wanaamini hivyo wakati si kweli.!

Hiyo ndiyo hisitoria fupi ya Kijiji cha Tanangozi kuhusishwa kuwa inaongoza kwa watu kula nyama ya mbwa.

Pengine kinachowafanya watu waamini hivyo, ni kutokana na historia iliyopo inayodaiwa kuwa nyama ya mbwa ni kitoweo kwa baadhi ya watu wa jamii hiyo.

Historia hiyo ilikolezwa na wazungu walipokuwa wakipita katika maeneo mbalimbali ya mkoani Iringa na kuwakuta wenyeji wakila chakula ambapo waliwahoji wanakula nini.

Kwa mujibu wa maelezo hayo, chakula kikuu cha jamii ya Wahehe kwa wakati huo, ilikuwa ni ugali na mboga maarufu yalikuwa ni maharage.

Wahehe maharage kwa lugha yao, huita `dogi,' hivyo, inasemekana baada ya kuulizwa wanakula nini, waliwajibu hao wazungu kuwa wanakula `ugali kwa dogi.'

Wazungu waliposikia wanakula ugali kwa `dogi,' wakatafsiri kuwa wanamaanisha kuwa wanakula ugali kwa nyama ya mbwa kwa kuwa mnyama huyo kwa lugha ya Kiingereza, huitwa `dog.' Kuanzia hapo, ndipo uvumi huo wa jamii hiyo kuwa hula nyama ya mbwa, ukasambaa kama moto wa nyikani na umendelea kusimama hivyo hivyo mpaka sasa licha ya kwamba hauna ukweli wala ushahidi wowote.

Kwa mfano, ukimkuta mtu wa jamii hiyo ambaye hajatoka nje ya mkoa huo na ukamuuliza suala hilo, utashangaa akikutalia kata kata kuwa hajawahi kusikia wala kumshuhudia mtu wa jamii yao akimfanya mbwa kitoweo, bali wengi hupata taarifa hizo baada ya kutoka nje ya mkoa wao.

**Ukweli ulivyo**

Kimsingi, jamii hiyo hufuga mbwa kwa ajili ya ulinzi katika makazi yao na kuwatumia kwa kuwindia wanyama kama swala, sungura, digidigi na kadhalika kama ilivyo kwa jamii nyingine hapa nchini.

Makala hii imeandikwa na mmoja wa wazaliwa wa Kijiji cha Tanangozi, Wilaya ya Iringa Vijijni mkoani Iringa na kusoma elimu ya msingi katika Shule ya Tanangozi.

# Rais Dk. Samia a mioyo ya wanaw

## Kukutana na BAWACHA

Na Mwandishi Wetu

JUMATANO iliyopita, dunia iliadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wanawake ambayo ilikuwa na kauli mbiu 'Ubunifu na Teknolojia: Chachu ya Usawa wa Kijinsia.'

Wanawake wa kada mbalimbali, walipaza sauti zao wakieleza namna ambavyo teknolojia ikitumika vizuri inaweza kumkwamua mwanamke na jamii kwa ujumla.

Pamoja na mengi yaliyozungumzwa kuhusu teknolojia, wanawake waliojumuika katika viwanja vya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), walimzungumzia mwanamke mwenzao ambaye pia ni Mkuu wa Nchi, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ya kipekee.

Mwanaharakati wa Haki za Binadamu nchini, Dk. Hellen Kijo-Bisimba, anamzungumzia Dk. Samia kama mwanamke wa shoka wa kuigwa.

la Wanawake wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), mkoani Kilimanjaro, ambako alialikwa kama mgeni rasmi kwenye maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake Duniani.

Anasema pamoja na kwamba mfumo wa vyama vingi vya siasa ni suala la kikatiba, katika hali ya utendaji mambo ni tofauti kwani imekuwa kama uadui.

"Nimemsikia anasema anataka kujenga nchi iliyo pamoja, na ndivyo inavyotakiwa. Nchi gani unaishi unaogopa kuingia kwenye vyama," anasema.

Anasema Rais kama kiongozi wa wananchi wote, anawajibika kuwakumbatia wote bila kujali itikadi za vyama, dini wala kabila.

"Alichofanya Rais, nimemfurahia na nikasema ametuonyesha tofauti ya uongozi kati ya mwanamke na mwanaume na hii inaweza kumjengea msingi mzuri sana," anasema.

Dk. Hellen anazungumzia maombi ya kufufua mchakato wa Katiba akieleza kuwa anatamani Rais Samia aongoze ajenda hiyo na



Mgeni rasmi, Profesa Veridiana Masanja, akizungumza wakati wa maadhimisho hayo ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya TGNP mwishoni mwa wiki iliyopita.

Anasema utendaji wake umedhihirisha utofauti wa namna ya kushughulikia mambo kati ya mwanaume na mwanamke.

Anasema wakati wa Uchaguzi Mkuu wa vyama vingi mwaka 1995, mfumo huo ulichukuliwa kama ni uadui, dhana ambayo anasema Dk. Samia anaifuta.

Anasema kitendo cha Mkuu wa Nchi na Mwenyekiti wa Chama kinachoongoza dola kujumuika kwenye jukwaa la wanawake wa chama cha upinzani, ni jambo la kwanza na lenye maana kubwa kwa ustawi wa nchi.

Itakumbukwa kwamba, Jumatano iliyopita, Rais Samia alijumuika na Baraza

kuihitimisha kwa manufaa ya nchi.

"Ningetamani aliongoze hilo ili aweke alama yake yeye kama Rais mwanamke kwamba nimeweza kufanya kitu kama hiki. Atuletee kitu cha tofauti, kitu mbadala na vitu ambavyo vimewahi kutokea," anasema.

### Miaka miwili madarakani

Dk. Hellen anazungumzia miaka miwili ya Rais Samia madarakani akisema aliingia kuongoza nchi wakati mwafaka.

Anasema ameingia madarakani katika kipindi kigumu na kwamba kile ambacho wananchi walikihitaji amekifanya.

"Kwa ile hali ambayo tulikuwa





Mwenyekiti wa Bodi ya TGNP, Gemma Akilimali (kushoto), Profesa Veridiana Masanja (mwenye kot Lilian Liundi na Mwakilishi wa UN Women nchini Tanzania, Hodan Adou, wakitembelea maonyesho (Picha: Mpigapicha Wetu.)

tumefikia, nadhani alikuwa ni mtu muafaka kuneutralize (kusawazisha) na kufanya hali iwe nzuri," anasema.

Anasema Rais Samia amefanikiwa kuachia baadhi ya watu ambao walikuwa wamefungwa na kurudisha akaunti za fedha zilizokuwa zimefungwa, jambo ambalo anaeleza kuwa ni zuri na haki za watu.

Hata hivyo, anasema wananchi wana mambo ambayo wangetamani yafanyike haraka na kwamba ni kwa kuwa wameyadai kwa muda mrefu.

"Suala kama la Katiba na sheria mbaya ziondolewe...tunatamani kama anaweza afanye sasa maana anaweza akaja mwingine

tukarudi kule kule. Kwa hii miaka miwili tumekuwa na kauhuru fulani kazuri sana," anasema.

Kuhusu maendeleo, Dk. Helen anasema miradi mikubwa inaendelea kutekelezwa jambo ambalo linadhihirisha kwamba mwanamke anaweza kufanyakazi nzuri.

Anasema pamoja na kwamba baadhi ya watu wanalalamikia mikopo inayochukuliwa na serikali, utekelezaji wa miradi mikubwa unaonyesha fedha hizo zinakopelekwa.

"Tukiweza kupata umeme nchi nzima kitakuwa ni kitu kizuri kama ambavyo tunaona mtandao mkubwa wa barabara za lami... tulikuwa tunaambiwa tutatoka Mtwara kwa

Jamii

# anavyogusa wake

## kwakoleza chachu



i jeupe), Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, ya wanawake katika viwanja vya TGNP.

barabara hadi Bukoba tukawa tunashangaa, lakini vitu kama hivyo vinawezekana," anasema.

Naye Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawenza, anampongeza Rais Samia kwa kuongea na wanawake kupitia jukwaa la BAWACHA, ni chachu ya kuleta mabadiliko ya uongozi katika jamii.

Anasema kitendo hicho kinajenga mahusiano miongoni mwa wananchi na kwamba kitaamsha nguvu ya mashauriano na kuwaleta watu pamoja.

"Ameenda kuimarisha ustawi wa vyama vya siasa nchini na amekuja kuimarisha mahusiano yanayojengeka katika misingi ya uongozi bora katika nyanja zote," anasema.

Naye Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake Wakiislamu Tanzania, Shamim Khan, anapongeza hatua hiyo ya Rais Samia akieleza kwamba amefanya tendo la kidemokrasia.

"Ndiyo demokrasia; yeye kachaguliwa na wanawake wote bila ya kujali chama. She is a super woman (Ni mwanamke hodari). Malumbano yapo katika mawazo na hii ndiyo demokrasia," anasema.

Anamwelezea Dk. Samia kama mwanamke anayefanya mambo mengi kwa manufaa ya makundi yote nchini bila kujali jinsia.

"Ni mwanamke shupavu, hana majivuno na mimi nasema mwaka 2025 tusimwache. Na ametuonyesha njia wanawake wengine kwamba tuthubutu. Elimu anayo, uwezo anao na ni mwanamke," anasema.

Anasema kwa utendaji wa Dk. Samia, hana wasiwasi kwamba mwaka 2025 'njia ni nyeupe' kwake kwa kuwa ameonyesha uwezo mkubwa.

Anasema serikali ya awamu ya sita imegusa sekta zote akitolea mfano wa afya, miundombinu, maji na nishati hivyo anawataka wanawake na wanaume wenye umri wa kushiriki uchaguzi wasimwache Rais Samia.

Mwanamke mbobevu wa Hisabati, Profesa Veridiana Masanja, anamwelezea Dk. Samia kama kiongozi wa mfano akitolea historia ya Chama cha Demokraisa na Maendeleo (Chadema) namna ambavyo maandamano yake yalivyogharimu maisha ya wananchi.

Anasema maandamano yalizorotesha ustawi wa mambo mengi na kwamba awamu ya tano kuzuia mikutano ya hadhara ilileta butwaa kwa vyama vya upinzani, jambo ambalo lilisababisha ufa kati wananchi na serikali.



Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Liundi, akizungumza katika maadhimisho hayo.



Anatoa mfano kwamba Jimbo la Arumeru Mashariki ambalo lilishikiliwa na upinzani, liliathirika na maandamano ya Chadema na hawakupata maendeleo kutokana na chama hicho kususia vikao mbalimbali vya serikali.

"Nampongeza sana Rais Samia kwa kukubali mwaliko wa BAWACHA...hatuwezi kusema sisi ni nchi ya amani kama hatuko tayari kusikiliza reconciliation (maridhiano), hata ndugu wa tumbo moja huwa wanagombana lakini mazungumzo huwaleta pamoja," anasema.

Anasema alichokifanya Rais Samia ni hatua muhimu ambayo itaboresha mambo mengi nchini.

### Wanawake na teknolojia

Katika maadhimisho ya mwaka huu, wanawake wamepewa mbinu za kuitumia teknolojia kwa faida badala ya kuchochea ukatili wa kijinsia.

Aidha, wanaume wamefundishwa kuitumia kuelimisha na kukemea ukatili badala ya kuitumia kufanya udhalilishaji kwa wanawake.

"Badala ya kutumia teknolojia, hasa mitandao ya kijamii kufanya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia, nitoe hamasa kwa jamii kutumia teknolojia hii kuelimisha jamii kuachana na vitendo hivyo na kuchukua hatua ili kuvitokomeza," anasema Lilian Liundi, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP.

> **Ni mwanamke shupavu, hana majivuno na mimi nasema mwaka 2025 tusimwache. Na ametuonyesha njia wanawake wengine kwamba tuthubutu. Elimu anayo, uwezo anao na ni mwanamke...**

Wanaharakati wa masuala ya kijinsia wanaitaja matumizi ya teknolojia na hususani mitandao ya kijamii kama nyenzo muhimu ya kutoa elimu na kukemea udhalilishaji. Kadhalika, wanaeleza kwamba teknolojia imerahisisha upatikanaji na utoaji wa taarifa hivyo ni silaha inayoweza kuwainua wengi kiuchumi na kijamii kama itatumika vizuri.

Kutokana na nafasi hiyo, Liundi anatoa rai kwa wanasayansi kubuni vifaa vitakavyosaidia katika harakati za kutokomeza ukatili wa kijinsia na kuboresha matumizi hayo kwa manufaa.

"Niwaase pia mabinti zetu na wanawake wenzangu muache kuweka mitandaoni picha za utupu kwani kwa kufanya hivyo pia ni kuchochea ukatili kwa watoto wa kiume na wanaume na kuwapa matamanio yasiyo na ulazima," anasema.

Jamii



# Utamaduni mpya Ruangwa usaidie maendeleo ya elimu

Na Abdul Mitumba, Ruangwa

ENZI na enzi, jamii ya watu wa Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, hawakuwa na utamaduni wa kucheza ngoma nyakati zote.

Ngoma zilishuhudiwa nyakati za kiangazi hasa kipindi cha mavuno au wakati wa sherehe za jando na unyago.

Lakini sasa mambo yamebadilika. Jamii hii imetawaliwa na ngoma, vigodoro na kila aina ya sherehe za wakati wote zinazoambatana na uundwaji wa vikundi visivyo rasmi kisheria, lakini vinavyokusanya fedha na michango ya vitu vingine ambayo tija yake katika elimu za watoto bado haijaonekana wazi kama Mwandishi Wetu anavyofafanua zaidi.

Nafikiri huu ni utamaduni mpya. Kila kaya, kila familia inajikuta ikiwa katikati ya shughuli zinazoambatana na sherehe za ngoma na midundo mizito ya muziki, maarufu kama vigodoro.

Hakika kwa jamii ya wana-Ruangwa imebadilika, huu ni utamaduni mpya. Muziki na ngoma za kitamaduni maarufu kama Likundumbwi na miziki ya singeli, vinatawala anga karibu yote ya wilaya hii.

Ukisikiliza kwa makini midundo yenyewe na jinsi wana-Ruangwa na jamii inayowazunguka wanavyokuwa 'bize', utadhani kwao sherehe ni zaidi ya mambo yote ikiwemo muda wa uzalishaji mali, maana utawaona wakitamba kila pembe ya wilaya.

> **Kindamba kwa sasa ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga huku nafasi yake ikichukuliwa na Dk. Francis Michael....**

Wakati mwingine wingi wa matukio ya sherehe, huvuruga hata mikutano ya hadhara ya kimkakati ya kupeana maelekezo kwa ajili ya shughuli za kimaendeleo.

Ukitaka kuuliza kama shughuli hizo ni za aina gani hasa, utaambiwa ni mahafali ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi (darasa la saba) au wakati mwingine ni sherehe za kuhitimu elimu ya awali.

Lakini unajiuliza, aina hiyo ya sherehe si huwa zinafanyika shuleni au vyuoni tena kwa pamoja!? Utaambiwa Ruangwa ni tofauti, siku hizi kila mzazi au mlezi anamfanyia mwanaye mahafali nyumbani!

Katika baadhi ya maeneo, utaambiwa sherehe za kumbukizi ya siku ya kuzaliwa mtoto au mtu mzima.

Hapo sasa pana hadi sare achilia mbali muziki mnene na vikundi maalum, ambapo wana vikundi hivyo wanachangishana fedha nyingi na vitu vingine kadha wa kadha.

Kibaya zaidi na cha kushangaza kwenye vikundi hivyo, wanawake hupigana vijembe hatari. Katika mtaa mingine utakutana na sherehe za watu waliochezwa pamoja yaani unyago.

Uchunguzi uliofanywa na Mwelekeo unaonyesha, kwamba kwenye aneo hili kuna vibweka, kiasi kwamba wakati mwingine ni vigumu kusimulia.

Kwa ufupi, eneo hili linahusisha sare za wana vikundi, muziki mzito, vyakula vya vingi sana na pombe za kila aina. Kama ni bia sawa, kangara au uraka yaani pombe nayotenegezwa kwa mabibo yaliyoiva. Vyote huwa vinapatikana na kutumika.

Funga kazi ni katika ndoa na harusi. Hapo ndipo itakapowajua watu wa jamii hii iliyobadilisha utamaduni, ndipo utakapowatambua vizuri.

Kila kitu ambacho hakifanyiki kwenye Birthday Party, unyago na mahafali, kwenye tukio hilo utakipata na ziada yake.

Inawezekana ni utamaduni mpya ambao wana-Ruangwa wameamua kuuishi sasa, lakini kinachoshangaza ni pale inapofika Januari hadi Machi ya kila mwaka, wakati ambao unalazimisha watoto kwemda kuanza mwaka wa masomo.

Au wakipelekwa ni kwa kuchelewa na wakati mwingine wakiwa hawana mahitaji muhimu shuleni.

Sababu ni kwamba, wazazi wakiwemo wana vikundi, wanakuwa wamemaliza fedha na vyakula kugharamia shughuli licha ya kuaminishwa kuwa kuna michango wanachangishana.

Afisa Maendeleo ya Jamii Idara ya Vijana wa Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Mwinyi Jalala anasema, kuwepo kwa vikundi hivyo ni sehemu ya uimarishaji wa jamii, lakini akavitaka kutumia vizuri fedha wanazochangishana ikiwa ni pamoja na kusomesha watoto.

"Najua fika kwamba, vingi kati ya vikundi hivyo havijasajiliwa. Lakini hilo siyo tatizo, wito wangu ni kwamba pamoja na malengo mengine mengi, lakini naomba kipaumbele cha kwanza kiwe kugharamia elimu ya watoto wetu," anasema.

Jalala anasema kila jamii au familia yenye watoto waliosoma na kuelimika ni rahisi kujibu maswali mengi yakiwemo ya ujinga na umaskini.

Afisa Ufuatiliaji na Tathmini wa Asasi ya kiraia ya Kuunganisha Vijana Kimaendeleo Ruangwa (AKUVIKIRU), Bahati Mtapa, anasema, jamii ya Ruangwa imeingia katika utamaduni mpya wa sherehe sizizokoma, lakini ikitumia vizuri utamaduni huo, inaweza kujikomboa kiuchumi.



Afya



# Je; wajua athari za kuangalia runinga kwa muda mrefu?

TELEVISHENI au runinga, ni chombo muhimu kwa binadamu kwa ajili ya kupata habari, matukio, burudani na kuelimisha kwa ujumla.

Hata hivyo, pamoja na umuhimu wake huo, chombo hicho kina madhara makubwa kwa binadamu hususan kwa yule anayetumia muda mwingi kuangalia runinga.

Inawezekana baadhi wameshasikia kwa kusoma katika makala mbalimbali kuhusiana na madhara hayo, lakini nasi tumeona ni vema tuendelee kuielimisha jamii ili kupunguza tatizo hilo.

Imeelezwa kwamba watu wanaotazama runinga kwa saa tatu au zaidi kila siku, wako katika hatari ya kuaga dunia mapema kuliko wale wanaotazama kwa muda mchache.

Uchunguzi uliochapishwa katika jarida la The American Heart Association nchini Marekani umebaini kuwa, utazamaji sana wa runinga, ni tabia ya watu wasio na kazi za kufanya na kuna ongezeko la mienendo ya kila aina ya tabia za kukaa tu.

Mtafiti Mkuu, Miguel Martinez-Gonzalez, ambaye ni Profesa wa Chuo Kikuu cha Navarra kilichoko Pamplona nchini Uhispania, alisema katika taarifa ya shirika hilo.

"Matokeo ya utafiti wetu ni sambamba na utafiti tuliowahi kufanya, ambapo muda unaotumiwa kutazama runinga uliolinganishwa na idadi ya vifo vinavyotokea kwa sababu hiyo," taarifa ya Profesa Martinez-Gonzalez, ilifafanua.

Watafiti hao waliwachunguza vijana wadogo 13,284 kutoka Uhispania wenye afya na waliohitimu chuo kikuu kuhusu aina tatu ya tabia za kukaa tu na hatari ya kuaga dunia kutokana na sababu zote, muda wa kutazama runinga na muda wa kuendesha gari.

Watafiti hao waliwashirikisha vijana wenye umri wa wastani wa miaka 37 ambapo asilimia 67 walikuwa wanawake. Kwa mujibu wa utafiti huo, vijana hao walifuatiliwa kwa takriban miaka 8.2 na mwishowe, vifo 97 viliripotiwa.

Kati ya vifo hivyo, 19 vilitokana na mishipa na moyo, 46 kutokana na saratani na 32 vilitokana na sababu nyinginezo.

Utafiti huo ulionesha hatari kubwa ya kuaga dunia ilikuwa mara mbili zaidi kwa washiriki walioripotiwa kutazama runinga kwa saa tatu au zaidi kwa siku ikilinganishwa na wale waliotazama kwa saa moja au chini ya hapo. Aidha, hatari hii mara mbili zaidi ilidhihirishwa pia baada ya kutoa hesabu ya safu kubwa ya vigezo vingine vinavyohusiana na hatari kubwa ya kuaga dunia.

Hata hivyo, watafiti hao hawakupata ushirikiano kati ya muda unaotumiwa na mtu anayeendesha gari na hatari kubwa ya kuaga dunia mapema kutokana na sababu hiyo.

Lakini, watafiti hao walishauri utafiti zaidi unapaswa kufanywa ili kuthibitisha ni athari zipi zilizopo kati ya kuendesha gari katika viwango vya vifo na pia kutathmini taratibu za kibailojia zinazoweza kueleza uhusiano wa vifo hivyo.

"Kadiri watu wanavyoendelea kuzeeka, na tabia ya kukaa bila kufanya kazi pia huongezeka na muda huo hutumiwa zaidi kuangalia runinga. Hali hii husababisha mzigo mkubwa katika ongezeko la matatizo ya kiafya yanayoambatana na kuzeeka," Mtafiti Martinez-Gonzalez, alifafanua.


**Matokeo ya utafiti wetu ni sambamba na utafiti tuliowahi kufanya, ambapo muda unaotumiwa kutazama runinga uliolinganishwa na idadi ya vifo vinavyotokea kwa sababu hiyo...**



"Matokeo ya utafiti wetu yanapendekeza watu wazima wajihusishe katika mazoezi ya viungo, waache kukaa tu kwa muda mrefu na wapunguze kutazama televisheni kwa zaidi ya saa mbili kila siku."

**Imeandaliwa na Mwandishi Wetu kwa msaada wa Mitandao**

## Kilimo



# Wakulima wa ufuta walia na wizi wa mazao sokoni

**Na Mwandishi Wetu, Lindi**

MOJA kati ya mambo yanayolalamikiwa na wakulima wa zao la ufuta mkoani Lindi ni wizi wanaofanyiwa kila wanapokwenda sokoni kupima ili kuuza mazao yao.

Wakulima wengi kama siyo wote, huuza mazao yao katika maghala ya vyama vya ushirika vya msingi (AMCOS) ambako wanasema makarani wa vyama hivyo, wanawavuruga na kuwaibia ufuta wao hivyo kupata fedha kidogo wakati wanauza mazao mengi. Katika makala haya ya kilimo Mwandishi Wetu, ABDUL MITUMBA anafafanua zaidi.

BAADHI ya wakulima wa zao la ufuta mkoani Lindi, wamesema wamechoshwa na vitendo vya wizi wa mazao yao ikiwemo ufuta, unaofanywa na makarani kila wanapokwenda kupima katika maghala madogo vya Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS).

Hali hiyo imewasukuma na kuazimia kwamba kama hakutakuwa na mabadiliko, msimu huu watauza ufuta wao wote kwa wafanyabishara maarufu kama 'Chomachoma' mashambani ili kukwepa wizi unaofanywa na baadhi ya makarani hao.

Wakulima hao wanasema, hatua ya kuuza ufuta kwa 'chomachoma' haina lengo la kukwepa makato ya asilimia mbili ya fedha za serikali na kwamba inakuja baada ya kupita zaidi ya misimu mitatu ya kuvumilia wizi wanaofanyiwa na makarani kwa kuchezea mizani.

Wakizungumza na Mwelekeo kwa nyakati na mahali tofauti ndani ya Wilaya za Liwale, Nachingwea na Ruangwa zinazolima zao la ufuta kwa wingi mkoani Lindi, wakulima hao wamedai kuwa uvumilivu umefika kikomo na kwamba dawa pekee ni kuuza ufuta ukiwa bado mashambani ambako wafanyabishara wamekuwa wakiwatembelea.

Ahmed Njuwalile, mkazi na mkulima wa Kijiji cha Makata wilayani Liwale, anasema, uchunguzi waliofanya kwa misimu mitatu mfululizo, wamejiridhisha pasipo na shaka kwamba makarani wanawaibia ufuta wao.

"Tumewahi kufanya majaribio kadhaa. Mfano, mkulima anakwenda na ndoo zake sita za ufuta zenye ujazo wa kilo 20 kila moja na kupima kwa makarani wa AMCOS anapata kilo 116. Lakini mwingine akienda na kiwango kama hicho hicho, ataambiwa kilo 105. Sasa swali linakuja, kilo nyingine huwa zinakwenda wapi?" Alihoji Njuwalile.

Mkulima mwingine aliyejitambulisha kuwa ni Amina Majenea wa Kijiji cha Lionja wilayani Nachingwea, amesema "msimu huu wakulima tumekubaliana hatutapeleka ufuta wetu sokoni hadi tuhakikishiwe uwazi katika upimaji."

Anasema, wizi unaofanywa na mawakala ni kama mtandao ulioandaliwa kikamilifu kwa lengo la kuwaibia wakulima kwa kisingizio kwamba mizani inayotumika ni ya muda mrefu.

> **Tunajua kwamba kwa kuuza ufuta kwa chomachoma, serikali itakosa mapato kutoka kwetu lakini tunaamini itapata kupitia kwa hao tutakaowauzia....**

Kauli hiyo imeungwa mkono na Juma Ngonde, mkulima wa Kijiji cha Machang'anja, wilayani Ruangwa, ambaye anasema wakulima watauza mazao yao kwa chomachoma hata msimu wa zao la korosho ukifika kwa sababu makarani wanawaibia bila woga.

"Tunajua kwamba kwa kuuza ufuta kwa chomachoma, serikali itakosa mapato kutoka kwetu lakini tunaamini itapata kupitia kwa hao tutakaowauzia, maana watauza mnadani ingawa ili wauze ndani ya wilaya ni lazima Serikali ifanye udhibiti wasitoroshe ufuta nje," amesema Bw.Ngonde.

Akizungumzia madai ya wakulima hao, Katibu wa Chama cha Ushirika cha Msingi cha Nanambu, kinachoundwa na vijiji vya Nandandara, Namkonjera na Mbuyuni, Fadhili Ndauka, amekiri kuwepo kwa malalamiko ya wakulima kuibiwa ufuta wao.

Anasema hata hivyo, madai hayo si makubwa kiasi cha wakulima kususa kuuza mazao yao Amcos.

"Tulichogundua ni kwamba, wizi umekuwa ukijitokeza kwa baadhi ya wakulima kuwatuma watu kwenda kupima mazao yao ambapo baadhi yao wamekuwa siyo waaminifu, wanagawanya mazao na kuyauza kwa majina tofauti, hali inayowapa maswali mengi wenye mazao yao," amesema.

Ndauka anasema kwa mfano, katika msimu uliopita, alikuja mtu na ufuta kilo 377, mzingo mmoja alipima na kuuza ukiwa na kilo 322 na kuandika jina la mwenye mzigo na kilo 50 akajipa yeye na kuandika kwa jina lake, lakini baadaye mwenye ufuta alilalamika sana akidai kuwa amepunnjwa.

Amesema, mbali na changamoto hizo, pia kuna tatizo la ubovu wa mizani inayotumika kupimia mazao ya wakulima kwa sababu imetengenezwa tangu miaka ya 1970 na kwa chiyo imepitwa na wakati.

"Ili kukabiliana na malalamiko yote haya, tunaiomba Serikali isaidie vyama vya ushirika kupata mizani za kisasa za kidigitali zenye uwezo wa kupima na kila mtu aweze kusoma kirahisi na kwa uwazi," amesema.

Ndauna anasema, mizani hizo zenye uwezo wa kupima kilo 250 hadi 350 kwa wakati mmoja zinauzwa kati ya Sh. 400,000 hadi Sh.500,000, wakati zile zenye uwezo wa kupima mazao kilo 400 hadi 500 zinauzwa ya Sh. 1, 700,000/=, kiasi ambacho Amcos zenyewe haziwezi kununua zaidi ya mzani mmoja.

Ni wazi kuwa, kama wakulima wataamua kuuza mazao yao kwa chomachoma, Serikali ya Wilaya ya Ruangwa itakosa fedha kiasi cha asilimia mbili katika kila kilo moja inayouzwa sokoni na wakulima bila kujali bei ya kilo moja itakuwa shilingi ngapi, ambazo ni ushuru kutoka kwa wakulima.

Kwa mfano, ikiwa wakulima watauza ufuta wakiwa mashambani bei ni kati ya Sh 1,000 na sh. 1,300 na hawatalipa kodi yoyote, wakati wakiuza mnadani kupitia vyama vya ushirika vya msingi, kilo moja huuzwa kwa bei ya kati ya Sh 1,700 na 2,300.

Gazeti hili lilipomtafuta Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Runali, Jahida Hassan, kuzungumzia malalamiko na hatua inayokusudiwa kuchukuliwa na wakulima msimu huu, alijibu kuwa alikuwa kwenye vikao mfululizo.

Runali ni Chama cha Ushirika cha Msingi kinachounganisha wakulima wa Wilaya za Ruangwa, Nachingwea na Liwale, lakini Jahida alisema angepata wakati mwingine angewasiliana na gazeti hili, ingawa hadi tunakwenda mitamboni, hakupatikana tena.

Mtaalam wa ushirika katika Idara ya Ushirika katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa, Patroba Andele, alipoulizwa kuhusu kuwepo kwa malalamiko hayo ya wakulima, alikataa kusema chochote kwa madai kuwa hana mamlaka ya kufanya hivyo.

Zao la ufuta ni moja kati ya mazao makubwa mawili kwa wakulima wa Mkoa wa Lindi, likilimwa zaidi katika Wilaya za Ruangwa, Liwale, Nachingwea na Kilwa. Zao lingine ni korosho.

**HABARI** MCHANGANYIKO

## Wafugaji Bungi walaumiwa kwa kuingiza mifugo mashambani

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA katika Kijiji cha Bungi visiwani humu, wamewalalamikia wafugaji ambao wamekuwa wakiingiza mifugo katika mashamba yao na kuharibu mazao.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi, baadhi ya wakulima hao, Rukia Ramadhan na Mwanamkuu Makame, wakazi wa Bungi Kiongoni, walisema wafugaji wamekuwa wakiwarejesha nyuma katika kuendelea na harakatai zao za kilimo ili kujipatia chakula.

Walieleza kuwa kila wanapojitahidi kulima, wafugaji hao bila ya huruma huiingiza mifugo kwenye mashamba yao na kuharibu mazao.

"Sisi watu wa vijijini, kazi zetu kubwa mbali ya ujasiriamali, pia tunajikita katika kilimo ambacho ndiyo tegemeo letu kubwa kujipatia chakula na mazao mengine, lakini kwa hali hii tunashindwa kutimiza malengo yetu," alisema Rukia.

Akizungumzia suala hilo, Sheha wa Shehiya Bungi, Vuai Ramadhan Vuai, alisema ni kweli wafugaji wamekuwa wakiingiza mifugo yao katika mashamba na kusababisha uharibifu mkubwa wa mazao ya wakulima.

''Kilimo ni kazi moja ngumu sana na unapoingiza mifugo yako katika shamba unamharibia mkulima, ni vyema wakaache tabia hiyo," alisema Sheha Vuai.

"Kesi nyingine huzimaliza hapa hapa katika ofisi yangu, lakini kuna nyingine nazifikisha katika kituo cha polisi na hivi sasa tunavyozungumza, kuna kesi tatu zipo mahakamani," alisema.

# RC aagiza halmashauri kuwashirikisha wapinzani

**Na Claud Gwandu, Arusha**

MKUU wa Mkoa Arusha, John Mongella, ameziagiza halmashauri zote za mkoa huu, kushirikiana na vyama vya upinzani ikiwa ni kuunga mkono jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, za kuleta maridhiano ya kisiasa nchini.

Amewataka viongozi wa halmashauri hizo kuanzia ngazi ya mkoa hadi vijijini, kushirikiana na vyama vyote vya kisiasa ili kuharakisha maendeleo ya wananchi.

Akizungumza katika Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) juzi, Mongella alisema suala la mariadhiano ni la kila mmoja na halipaswi kuachiwa ngazi za juu pekee vinginevyo, halitakuwa na maana.

"Ni kwa msingi huo naagiza,viongozi katika ngazi zote kwenye halamshauri hadi mkoa washirikiane na hawa wenzetu ili kwa pamoja tusonge mbele," alisisitiza Mongela.

"Tutakapowashirikisha itasaidia kupata mawazo mbadala na kuboresha pale panapotakiwa kuboreshwa,'' alisema.

Katika kikao hicho, Mkuu huyo wa mkoa pia alizindua kitabu cha miaka miwili ya mafanikio ya Rais Dk. Samia ambaye aliingia madarakani Machi 19, 2021 kufuatia kifo cha mtangulizi wake, Dk. John Magufuli aliyefariki dunia Machi 17, mwaka 2021.

Alisema katika kuadhimisha miaka miwili ya Dk. Samia



**Mkuu wa Mkoa Arusha, John Mongella**

> **Lakini tunashukuru Rais katuwezesha kuwa na mazingira ya uhuru na usalama ambayo yamesaidia Mkoa wa Arusha kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 533...**

kuwa Rais, mkoa huo uliamua kuadhimisha miaka hiyo kwa kutoa kitabu kinachoelezea kazi zilizofanywa mkoani kwa miaka miwili.

"Lakini tunashukuru Rais katuwezesha kuwa na mazingira ya uhuru na usalama ambayo yamesaidia Mkoa wa Arusha kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 533 sawa na asilimia 107.13 katika kipindi cha miaka miwili na lengo la mwaka huu kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 411," alisisitiza.

Alisema kitabu hicho cha miaka miwili ya uongozi wa Rais Dk. Samia, kimeelezea maboresho mbalimbali katika huduma za kijamii ambako katika sekta ya afya, ameboresha Hospitali za Wilaya ya Monduli, Longido, Karatu na Ngorongoro, ili wananchi wapate huduma bora za afya, ikiwa ni pamoja na kupunguza vifo vya kinamama na watoto.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa Arusha, Zelothe Steven, alisema Rais Samia amefanya kazi ambayo hawajawahi kuiona katika kipindi cha miaka miwili.

"Mtangulizi wake, Rais John Magufuli, alifariki dunia ila Rais Samia hakutetereka na Taifa limebakia katika umoja wake na amesimamia Muungano ulio imara," alisema na kuongeza:

" Miradi mikubwa iliyokuwa inatekelezwa inaendelea na hakuna hata mmoja uliozorota, usafiri wa anga, majini, afya na mengine mengi inaendelea vizuri," alisema.

Alisisitiza kuwa hata watalii wanaofurika hivi sasa ni ubunifu wa Rais Samia kwa kutumia Filamu ya Royal Tour ambayo imegusa kila mahali na amekuwa mstari wa mbele kupambana na umaskini, maradhi na ujinga.

Kuhusu maridhiano ya kisiasa, Mwenyekiti huyo wa CCM Mkoa wa Arusha, alisema Rais Samia ameishangaza dunia kwa kuingia maridhiano ya kisiasa kwa sababu watanzania wote wanajenga nyumba moja na hakuna sababu ya kugombea fito.

Kuhusu mmomonyoko wa maadili nchini, RC Mongella aliwataka viongozi wa dini kuungana katika kukemea mmomonyoko huo hasa vitendo vya ushoga.

Alisema pamoja vyombo vya dola kupambana ili kudhibiti tatizo hilo, lakini bado nguvu kubwa ya kila mmoja inahitajika.

Alisema mashoga wanatoka katika familia na wao viongozi wanatoka katika familia hivyo lazima familia zisimame imara kukemea vitendo hivyo.

"Mmomonyoko mkubwa wa maadili upo katika jamii yetu licha ya kujitahidi vyombo vya dola kupambana lakini sioni kama tutafanikiwa kama hatutachukua hatua zaidi," alisema.

Alitumia fursa hiyo pia kuwapongeza Baraza Kuu la Waislamu (BAKWATA) kuandamana kwa ajili ya kupinga udhalilishaji na unyanyasaji wa wanawake na watoto.

"Kitendo hiki kinapaswa kuigwa na kila mtu bila kujali itikadi zetu za vyama na dini sababu mwisho wa siku tunajenga nyumba moja," alisema.

# `Muhimu kwa wafayakazi kufahamu masuala ya kisheria'

**Na Mwandishi Wetu**

AFISA Utumishi kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Yussuf Mohammed Suleiman, amesema ni muhimu kwa wafanyakazi kufahamu masuala yao ya kisheria kwa kuwa husaidia kuondoa malalamiko.

Akitoa mada katika mafunzo ya Sheria ya Utumishi wa Umma yaliyowashirikisha wafanyakazi kutoka Wizara ya Maji, Nishati na Madini,Yussuf alisema hlo ni muhimu kwa kila mfanyakazi, lakini kwa wizara hiyo ni muhimu zaidi kwa sababu huduma zao nyingi zinategemewa na wananchi.

Hivyo alisema kutokana na umuhimu huo, ni wajibu wao kuzijua sheria za utumishi na kufuata miongozo ambayo itaondoa malalamiko kwa wananchi pale wanapokosa huduma.

'Sisi watumishi wa umma, tupo kuhakikisha kwamba mahitaji ya wananchi yanapatikana kupitia mfumo wa sheria ya utumishi wa umma, hivyo tufahamu hapo ulipo ni sehemu ya utumishi wa umma na kwamba kuna wananchi wanakutegemea hususan katika huduma zenu ambazo nyingi zinawategemea wananchi," alisema.

Mapema, akifungua mafunzo hayo, Mkurugenzi Idara ya Mipango na Ufuatiliaji, Mariam Issa Juma, alisema mafunzo hayo wameyaandaa kwa lengo la kukumbushana kuhusu sheria ambao ni utaratibu waliouweka kwa kila mwaka.

Hata hivyo, alisema kupitia mafunzo hayo ana hakika wafanyakazi hao watakuwa tayari kufanya kazi kwa kufuata misingi ya sheria na kuacha mazoea.


Wakitoa mada kuhusu wajibu wa kupambana na rushwa kwa watumishi wa umma, maafisa elimu kutoka Mamlaka ya Kudhibiti Rushwa na Uhujumu Uchumi, Yussuf Juma Slim na Saumu Ramadhan Haji, walisema uadilifu ni kitu ambacho kinatoa ngao katika utendaji kazi kwa watumishi wa umma.

Hivyo alisema kuchukua au kutoa rushwa, ni jambo ambalo lipo kinyume cha maadili yao katika kazi.

"Ili kukimbia matatizo, ni lazima mtumishi atekeleze jukumu ambalo anatakiwa kulifanya na wawe wazalendo na wenye kufahamu sheria, taratibu na miongozo iliyopo kwa mujibu wa sheria," alisema Yussuf.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki wenzake, Mussa Ali Kombo, alisema mafunzo hayo yatawasaidia na watajua taratibu mbalimbali za kiutumishi ikiwa ni lengo la kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mafunzo hayo ya siku moja, yaliandaliwa na Wizara ya Maji, Nishati na Madini na kuwashirikisha watendaji wote wa wizara hiyo yakiwa na lengo la kuwasaidia ufanisi katika kazi na kufikia malengo yaliyowekwa na wizara ya


MIAKA MIWILI YA MAMA
HONGERA SANA MAMA NA ASANTE TUANAKUOMBEA DUA KWA MWENYEZI MUNGU AKUPE MAISHA MAREFU, AFYA NJEMA NA AKUSIMAMIE KATIKA UONGOZI WAKO
MIRADI YA KIMKAKATI
Katuniz
KIMWELEKEO
@Muhidini Msamba
+255656122770
KWANINI UNASEMA MADRASA YENU YAMEKOLEA NAZI SHATA SHATA!?
RAIS WETU DK SAMIA SULUHU HASSAN KATUJENGEA MADARASA MAZURI HADI NATAMAI TUKAISHI HUKO
AWAMU HII TAMU SANA MTANI WANGU MAANA KILA GOLI KIMATAIFA MILIONI TANO
KWELI MTANI WANGU TUSIPO NENEPA AWAMU HII BASI SIJUI TUTANENEPA LINI TENA ,RAIS WETU DK SAMIA SULUHU HASSAN ANATUPENDA SANA
MIAKA HII MIWILI YA RAIS WETU DK SAMIA KAFANYA MAKUBWA SANA KAMALIZIA BWAWA LA MWALIMU NYERERE, SGR KWA KWELI TUNAJIVUNIA KUWA NA RAIS MCHAPAKAZI
KWELI RAFIKI SASA WATOTO WETU WANASOMA KWA RAHA MSTAREHE KWANI KAJENGA SHULE NZURI KILA KATA HAPA NCHINI
TUNATEMBEA KWENYE KAPETI HATA MITAANI KWETU KWELI MAMA ANATUJALI SANA
MSISAHAU MARIDHIANO NA VYAMA VYA SIASA
MBONA MIMI WAKATI NAPANDA SIJAONA KAPETI!?
WATOTO WA MJINI WANASEMA KACHEZA KAMA PELE
HAHAHA... ANAMAANISHA BARABARA ZA LAMI NA ZEGE
HAO WA ENZI ZENU RAFIKI SISI TUNASEMA KAUPIGA MWINGI, WALIOKIMBIA NCHINI WANARUDI KWA RAHA YA UONGOZI BORA WA RAIS WETU MPENDWA
JAMANI MSISAHAU VITUO VYA AFYA KAJENDA KIBAO
AHAAA... KAMA NI HIZO HATA KWETU NINAKOISHI ZIPO

# Amnesty yaonya matumizi ya risasi

**BAGHDAD, Iraq**

SHIRIKA la Kimataifa la Kutetea Haki za Binadamu (Amnesty International), limeonya kuhusu kuongezeka kwa matumizi ya risasi za mpira kunakofanywa na polisi dhidi ya watu wanaoandamana kwa amani ulimwenguni kote.

Hayo yameelezwa katika ripoti ya shirika hilo lenye makao yake mjini London, Uingereza iliyotolewa jana ikieleza kuwa matumizi ya risasi za mpira na silaha nyingine, dhidi ya watu wanaoandamana kwa amani yamesababisha wengi kupata majeraha ya macho na hata vifo.

Amnesty International imetoa wito wa kuwepo kwa udhibiti bora wa kimataifa wa biashara na matumizi ya vifaa hivyo vya polisi, vinavyojulikana pia kama 'silaza zisizo na madhara makubwa.'

Hayo yamo katika ripoti ya shirika hilo inayofuatia utafiti uliofanyika katika zaidi ya nchi 30, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo iliyopewa jina 'Jicho Langu Limelipuka', maelfu ya waandamanaji na watazamaji wamekuwa walemavu na wengine kadhaa wameuawa kutokana na uzembe wa matumizi mabaya na ya mara kwa mara ya silaha hizo katika kutekeleza sheria kandamiza dhidi ya maandamano ya amani.

Silaha hizo ni pamoja na risasi za mpira, vilipuzi vya mpira na mabomu ya kutoa machozi ambayo zilifyatuliwa moja kwa moja dhidi ya waandamanaji katika maeneo ya Amerika ya Kusini na Kati, Ulaya, Mashariki ya Kati, Afrika na Marekani. Amnesty International imesema kumekuwa na ongezeko la kutisha la majeraha ya macho, ikiwa ni pamoja na kupasuka kwa mboni ya jicho, kuchanika kwa eneo la ndani ya jicho na watu kupoteza kabisa uwezo wa kuona.

> **Kwa mujibu wa ripoti hiyo iliyopewa jina 'Jicho Langu Limelipuka', maelfu ya waandamanaji na watazamaji wamekuwa walemavu na wengine kadhaa wameuawa kutokana na uzembe...**

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, nchini Chile pekee, kuanzia Oktoba mwaka 2019, kulikuwa na zaidi ya visa 30 vya watu kupoteza uwezo wa kuona baada ya polisi kukabiliana na waandamanaji. Hayo ni kwa mujibu wa Taasisi ya Kitaifa ya Haki za Binadamu nchini humo.

Ripoti hiyo imesema waandamanaji wengine kwenye nchi kadhaa zilizofanyiwa utafiti pia mifupa yao na mafuvu yalivunjwa, walipata majeraha ya ubongo, kupasuka kwa viungo vya ndani ya mwili na kupasuka kwa mbavu. Kwa mujibu wa ripoti hiyo iliyoandikwa kwa ushirikiano na Wakfu wa Utafiti wa Omega, waandamanaji wengine pia waliuawa.

Shirika hilo la kimataifa la kutetea haki za binadamu limesema nchini Iraq, vikosi vya usalama vilifyatua kwa makusudi kabisa mabomu ambayo ni mazito mara 10 zaidi kuliko mabomu ya kawaida ya kutoa machozi dhidi ya waandamanaji, na kusababisha takribani vifo 24 mwaka 2019.

Ilieleza kuwa nchini Hispania, matumizi ya risasi zenye ukubwa wa mipira ya kuchezea mpira wa tenisi yalisababisha kifo cha kimoja kutokana na majeraha ya kichwa.

Hayo yalilezwa na shirika la Stop Balas de Goma, linalofanya kampeni ya kuzuia matumizi ya risasi za mpira. Mwanaharakati wa haki za binadamu anayefanya kazi na Amnesty International, Patrick Wilcken, alisema udhibiti unaofungamana na sheria ya kimataifa kuhusu biashara ya silaha zisizo na madhara makubwa na zenye hatari na miongozo madhubuti ya matumizi ya nguvu, zinahitajika haraka ili kupambana na unyanyasaji.

**DW**



**Polisi wa Iraq, wakiwatawanya waandamanaji mjini Baghdad kwa mabomu ya kutoa machozi. (PICHA: DW)**

## Wafungwa watoroka kizuizini Afrika Kusini

**CAPE TOWN, Afrika Kusini**

RAIA sita wa Zimbabwe wanaoshukiwa kuwa majambazi wakiwa na silaha, wametoroka kutoka kizuizini walipokuwa kwenye usafiri siku ya Jumatatu asubuhi baada ya wenzao kuwakabili polisi wa Afrika Kusini katika majibizano ya risasi.

Katika taarifa, polisi wa Afrika Kusini walitangaza msako wa kuwasaka washukiwa hao 'wenye silaha nzito' ambao waliwaachilia wafungwa sita wakati wa mapigano hayo ya risasi.

Shambulio hilo la kijasiri lilifanyika umbali wa kilomita 120 kusini mwa Beitbridge, mji wa mpakani karibu na Zimbabwe.

"Watu wanashauriwa kutowakaribia washukiwa kwa hali yoyote ile kwani wanachukuliwa kuwa hatari badala yake watoe ripoti kwa polisi," polisi wa Afrika Kusini walisema.

Zimbabwe ina idadi kubwa ya wahamiaji nchini Afrika Kusini huku raia wake wakiendelea kutoroka matatizo ya kisiasa na kiuchumi nchini humo.

Serikali ya Afrika Kusini imekuwa ikikabiliana na raia wa kigeni hasa Wazimbabwe wanaohusika na uhalifu wa kutumia nguvu.

**BBC**

## Madhehebu yalia na M23

**KINSHASA, DRC**

VIONGOZI wa madhehebu mbalimbali ya Kikristo mkoani Kivu Kaskazini wamezindua mpango wa kuhimiza amani na kuyahimiza makundi ya waasi likiwamo la wapiganaji wa M23 kusitisha mapigano.

Vyanzo kutoka mashirika ya kiraia katika maeneo mbalimbali wilayani Masisi, vilieleza jana kwamba vimeona waasi wa M23 wakiondoka katika mji mdogo wa Mweso, Kiuli, Malehe na kwenye milima ya kijiji cha Karuba.

Taarifa kutoka DRC zinaeleza kuwa misururu ya wapiganaji wameonekana wakiwa wamebeba mizigo na silaha. Hata hivyo, hawajaeleza kama walikuwa wanaelekea wapi.

Upande wa mashirika ya kiraia, ulielezea wasi wasi wake kufuatia hatua hiyo ya M23 ambayo imekuwa ikitajwa kuwa ni ujanja wa kuendelea kuvishikilia vijiji vingine.

Wakati huo huo, katika mkutano wao na vyombo vya habari, viongozi wa madhehebu mbalimbali mkoani Kivu Kaskazini walikutana jana na kujadili hali jumla ya usalama mkoani Kivu Kaskazini.

Katika mkutano huo, wakuu hao kutoka madhehebu mbalimbali ya kidini wamewataka wananchi kukuza amani ambayo ni njia pekee ya kuzima mzozo unaoendelea kufukuta kati ya serikali na kundi la waasi wa M23.

Hayo yanajiri siku moja baada ya ziara ya siku tatu ya wajumbe wa Baraza la Umoja wa Mataifa nchini Congo, waliolitaka kundi hilo la waasi wa M23 kuondoka na kuyaacha maeneo yote linalodhibiti.

**DW**



**Karibu katika duka letu ili kupata bidhaa halisi za Chama Cha mapinduzi**

**Tunauza:**

- Kaunda suti
- Shati
- Tisheti
- Magauni
- Weel cover
- Note book
- kalamu
- viatu
- Kofia
- n.k.

**Mawasiliano**

+255 733 768 825
info@umg.co.tz
www.umg.co.tz

**Tunapatikana**

Ofisi ndogo za CCM Lumumba

Jarida la MWELEKEO

# SOMA NA PAKUA GAZETI HILI BURE

Kupitia.

www.umg.co.tz


Mwelekeo
Leo yetu ndiyo kesho yetu
Dk. Samia: Vijiji vyote umeme mwaka huu
... Tundu Lissu sasa amkubali
Undani wa Wajumbe Sekretarieti ya NEC ya CCM
Nini kitatokea Ukraine Feb. 24

@jaridalamweleko



# Amri Saidi Sijawahi kukatishwa tamaa kufundisha soka

**Maisha yangu yametawaliwa na soka. Nimecheza kwa kiwango cha juu tangu niiliwa Maji Maji ya Songea hadi Simba. Hata nilipoanza kufundisha, najiona nina kila sababu ya kuendelea hadi nitakapoacha alama kubwa na ya kudumu....**

**Na Abdul Mitumba, Ruangwa**

MOJA kati makocha wazawa wanaofanya vizuri wakiwa kazini na mwenye ndoto kubwa ya kuja kuwa miongoni mwa makocha wakubwa na mwenye mafanikio katika soka ni aliyewahi kuwa beki wa Klabu ya Simba, Amri Said 'Jaap Stam'.

Stam ni jina kubwa katika soka barani Ulaya ,ambapo liliwika na kutamba likimwakilisha aliyekua mlinzi kisiki wa kati katika timu kadhaa za Ulaya ikiwemo Manchester United ya England na timu ya taifa ya Uholanzi.

Kama ilivyo kwa Amri Said, ambaye nyakati zake akicheza Simba, aliwika vilivyo ambapo alikua kisiki cha maana hadi mashabiki kumpachika jina la Jacob Stam 'Jaap Stam'.

Jaap Stam ambaye alizaliwa Julai 17, 1972 sasa amefikisha miaka 51 ambaye kwa naye amekuwa kocha.

Kwa Amri Said, Jaap Stam bado amekua kielelezo sahihi cha kuifanyakazi ya ukocha kikamilifu.

Kabla ya kutamba akiwa na Wekundu wa Msimbazi Simba, Amri aliwahi kukiwasha akiwa na kikosi cha Majimaji ya Songea hivyo kumpa kibali cha kutua Msimbazi.

Kama walivyo makocha wengi duniani, Amri alianza kazi ya kufundisha soka mwaka 2010 baada ya kufuzu mafunzo ya awali ya ukocha.

Kisha akaendelea na mafunzo ya ukocha ngazi ya kati (Intermidiet) mwaka 2014, mafunzo yaliyoratibiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) na kusimamiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) na kupata leseni ya daraja C.



Akizungumzia safari ya ukocha Amri anasema, mwaka 2016 alirudi tena darasani na kuhitimu mafunzo mengine ya CAF na kupata daraja la pili (B), hivyo kumwezesha kufundisha timu za Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Nikiwa kocha nimefundisha timu mbalimbali na kupata mafanikio makubwa, ambapo klabu niliyoacha alama ni Simba ambako nikiwa katika benchi la ufundi, nilishkiriki katika kuiwezesha timu kuwa bingwa bila kufungwa msimu wote," anasema.

Amefafanua kuwa msimu huo ulikuwa ni wa 2019/2020, Simba ilikua inanolewa na Kocha Mkuu raia wa Zambia, Patrick Phili.

Anasema, mbali na kufundisha Simba pia amewahi kuwa Kocha Mkuu kwa nyakati tofauti katika Klabu za Ndanda ya Mtwara, Mwadui ya Shinyanga, Mbao ya jijini Mwanza, Mbeya City na Biashara United ya mkoani Mara.

Kocha huyo anasema, katika maisha yake ya ukocha licha ya kukutana na changamoto kadha wa kadha, lakini hajawahi kukatishwa tamaa, kiasi cha kufikiria kuacha kufundisha soka.

"Maisha yangu yametawaliwa na soka. Nimecheza kwa kiwango cha juu tangu niiliwa Maji Maji ya Songea hadi Simba. Hata nilipoanza kufundisha, najiona nina kila sababu ya kuendelea hadi nitakapoacha alama kubwa na ya kudumu," anasema.

Anasema, kabla hajaanza soka la ushindani mwaka 2000 kama walivyo wachezaji wengi duniani, alianza kucheza timu za mitaani kabla ya kujiunga na Maji Maji na baadaye Simba,

Amri anaamini siku moja atakabidhiwa kufundisha moja kati ya timu kubwa za soka hapa nchini na hapo ndipo, Watanzania watakapojua uwezo wake na kukamilika kwa ndoto anayoendelea kuishi nayo.

Akizungumzia msimu wa Ligi Kuu ya NBC unaoelekea ukingoni, anasema ni ligi ngumu na bado haijawa wazi sana kwamba nani atakua bingwa, licha ya kwamba Yanga inaongoza kwa tofauti ya pointi nane mbele ya Simba.

# Conte mbioni kuondoka Tottenham Spurs



**LONDON, England**

KOCHA wa Klabu ya Tottenham Hotspurs, Antonio Conte anaweza kuondoka katika klabu hiyo haraka endapo atashindwa kuweka malengo ya siku za usoni.

Kauli hiyo imetolewa na mshambuliaji nyota wa zamani wa Blackburn Rovers, Chris Sutton ambaye pia ni mchambuzi wa soka.

Mkataba wa Conte (53), utamalizika mwishoni mwa msimu huu, huku Spurs ikiwa nje katika ushindani wa kuwania mataji kwenye mashindano.

Spurs ipo nafasi ya nne katika Ligi Kuu England, ambayo ni ya mwisho kwa timu kufuzu mechi za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Nadhani wanaweza kufikia uamuzi wa pamoja, ataondoka baada ya msimu kumalizika, lakini nimeshangazwa na mwenendo wa Spurs hivi sasa," alisema Sutton.

Sutton alisema, Muitaliano huyo ana nafasi ya kuamua kama atabaki Spurs akiwa na malengo ya kujenga timu imara au aondoke.

Conte aliipa Chelsea ubingwa wa Ligi Kuu England msimu 2016-2017 na Kombe la FA kabla ya kufukuzwa. Aidha baada ya kuipa taji la Italia Inter Milan msimu 2020-2021, alirejea Spurs kujaza nafasi ya Nuno Espirito Santo.

## Zaha katika mtihani mgumu kutoa uamuzi kwenda Al-Ittihad

**LONDON, England**

WINGA wa Crystal Palace, Wilfried Zaha yupo katika mtihani mgumu wa kutoa uamuzi baada ya kuahidiwa donge nono na Klabu ya Al-Ittihad ya Saudi Arabia.

Matajiri hao wameweka mezani pauni milioni tisa kutaka saini ya mchezaji huyo, lakini Palace imeweka ngumu.

Lakini tai hao, wameingia vitani kumshawishi winga huyo kubaki kwa maboresho ya mkataba ambapo wameahidi kumpa mshahara mnono.

Mshambuliaji huyo wa Ivory Coast, atakuwa nje ya mkataba majira ya kiangazi na anataka kuangalia mustakabali wake wa muda mrefu ndani ya klabu hiyo au vinginevyo. Mchezaji huyo ameahidiwa mshahara ambao utavunja rekodi ya klabu hiyo pauni 200,000 kwa wiki.

Saudi Arabia imepania kuboresha ligi yake baada ya klabu ya Al-Nassr, kumsajili nyota wa zamani wa Manchester United, Real Madrid na Juventus Cristiano Ronaldo.

Hata hivyo Zaha (30), anaweza kuikacha klabu hiyo kwa kuwa anataka kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya. Nyota huyo anawindwa na miamba ya soka Italia AC Milan.





## Manchester United haina mpango kukata rufani

**LONDON, England**

MANCHESTER United imesema, haina mpango wa kukata rufani kupinga kadi nyekundu ya kiungo wake Casemiro, aliyopewa katika mechi dhidi ya Southampton. Kiungo huyo raia wa Brazil, alilimwa kadi nyekundu ya moja kwa moja katika mchezo huo waliotoka suluhu, lakini Man United imesema haitakara rufani.

Casemiro aliyejiunga na Man United akitokea Real Madrid msimu uliopita wa majira ya kiangazi, amekua mchezaji tegemeo wa kikosi cha kwanza.

Mwamuzi Anthony Taylor alimpa kadi Casemiro kwa kosa la kumchezea vibaya Carlos Alcaraz, baada ya kwenda kujiridhisha kwa marudio ya msaada wa video. Casemiro atakosa mechi nne za mashindano ikiwemo ya robo fainali ya Kombe la FA dhidi ya Fulham, pia atazikosa mechi tatu za Ligi Kuu dhidi ya Newcastle United, Brentford na Everton.

"Casemiro amecheza mechi zaidi ya 500 katika ligi mbalimbali Ulaya, hakuwahi kupata kadi nyekundu, lakini sasa amepata mara mbili," alisema kocha wa Man United.

## Chelsea yajiandaa kufanya uamuzi mgumu

**LONDON, England**

CHELSEA inajiandaa kufanya uamuzi mgumu wa kuwatupia virago wachezaji 11 majira ya kiangazi, ili kujenga timu imara ya ushindani.

Kwa mujibu wa taarifa ya klabu hiyo, imekuja wakati wachezaji sita wako nje ya mkataba akiwemo kiungo nyota Mfaransa N'Golo Kante na Ethan Ampadu.

Pia wachezaji wengine watano watakuwa nje ya mkataba, hivyo Chelsea inaweza kutoa uamuzi mgumu wa kuachana nao ili kupata fursa ya kusajili wachezaji wapya kujenga timu bora.

Miongoni mwa wachezaji wanaotarajiwa kupigwa bei ni pamoja na Mason Mount, Christian Pulisic na Pierre-Emerick Aubameyang. Chelsea inaweza kuachana na Kante, majira ya kiangazi ingawa kuna taarifa klabu hiyo inataka kuanzisha mazunguzo ya mkataba. Msimu huu kiungo huyo hakutoa mchango kutokana na kuandamwa na majerahaya muda mrefu. Kuondoka kwa Aubemeyang, hakutashtua kwa kuwa anahusishwa na mpango wa kwenda kucheza Ligi ya Marekani. Cesar Azpilicueta anahusishwa kurejea Hispania baada ya kucheza kwa takribani miaka 10 Chelsea.



# Cheupe azitaka klabu zibadilike kwa vitendo

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), Ali Bakari Cheupe amesema ufike wakati klabu zibadilike kwa vitendo ambavyo vinachangia kuvunjika kwa michezo au kuchelewa kuanza.

Hayo aliyazungumza hivi karibuni mara baada ya kukamilisha upangaji wa ratiba ya Kombe la Shirikisho {FA} inayotarajiwa kuanza kesho.

Alisema tabia ya baadhi ya klabu ya kuleta ubishi usiofuata kanuni unaharibu mustakabali mzima wa mwenendo wa ligi na hata kuwafukuza wafadhili.

Mwenyekiti huyo alisema katika ligi zao, zimebarikiwa kupata udhamini lakini kwa mambo ambayo wanafanywa na klabu huenda wadhamini hao wakaoondoka.

"Klabu zinafanya mambo ambayo wanaona ni rahisi lakini wanaathiri wadhamini, kwa mfano hivi karibuni mchezo kati ya Ngome na Jang'ombe Boys tayari wadhamini wameshaweka vifaa vyao lakini haukuchezwa kwa sababu ambayo wakati mwingine inakua haina mashiko," alisema.

Alisema kama kweli wanataka maendeleo kwa klabu zao, viongozi wake wanatakiwa kuweka pembeni utashi binafsi na waangalie hatma yao ya baadaye.

"Kuna vitu tusichukulie kirahisi na tuwape ushirikiano wale ambao tunafanya nao kazi, unapoahirisha mchezo pasipo na sababu za msingi tunawatia gharama wenzetu," alisema na kuongeza, timu inafika uwanjani hazichezi ni lazima wabadilike ili tusiwafukuze wadhamini".

Naye Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi ya Shirikisho hilo, Hashim Salum alisema viongozi wa klabu wanapaswa kuwa makini katika kuhakikisha wanajenga matumaini kwa wadhamini ambao wamekuja kwa nia thabiti ya kusaidia mpira wao.

Hata hivyo alisema mfano hai na wa kuigwa ni huo wa Zanzibar Cable, ambao walidhamini Ligi Kuu miaka iliyopita lakini kutokana na heshima ambayo waliipata wamediriki kurudi tena kudhamini Kombe la Shirikisho.

"Mpira wetu tuutazame kurudi kwa Zanzibar Cable ni heshima, ili heshima hiyo iendelee kuonekana ni lazima klabu zicheze kwa nidhamu ya hali ya juu," alisema.

Aliwataka viongozi wa klabu na wadau wengine wa mchezo huo, wasiwe adui wa nafsi ili wawe na kitu bora na kulinda wadhamini wao.

## Kigogo CCM Tandahimba asaidia mipira shule sita

**Na Abdul Mitumba, Aliyekuwa Tandahimba**

CHAMA cha Mapinduzi (CCM) Tawi la Miembeni Kata ya Chaume Wilaya ya Tandahimba mkoani Mtwara, kimetoa mipira mitano kwenye shule nne za msingi na moja ya sekondari, ili kuinua ari ya wanafunzi, kupenda na kushiriki michezo mapema.

Shule za msingi zilizonufaika na msaada huo wenye thamani ya sh. 325,000 ni Chaume, Liponde, Mwelu na Juhudi wakati kwa sekondani ni Chaume ya Kata ya Chaume.

Akizungumza muda mfupi baada ya kukabidhi msaada huo, Mwenyekiti wa Tawi la Miembeni, Juma Kulyamba alisema amelazimika kusaidia watoto kwa sababu anaamini vipaji huanza kuonekana vijana wakiwa wadogo.

"Wote hapa ni mashahidi, kama kweli tunataka kuona na baadaye kuvuna vipaji vya watoto wetu katika michezo hususan soka ni lazima tuanze kuwasaidia wakiwa wadogo tena wakiwa shuleni," alisema.




**Katibu Tawala Mkoa Mjini Magharibi, Muhammed Abdalla akiwa kwenye picha ya pamoja na viiongozi mbalimbali wakiwemo viongozi vijana kutoka Vyuo Vikuu vya Zanzibar na viongozi wa Braza la Vijana mara baada ya kuyafunga mafunzo elekezi kwa viongozi vijana, yaliyoandaliwa na uongozi wa Raha Tv Online yaliyofanyika Ukumbi wa Zanzibar School Of Health kilichopo kwa Mchina Mwanzo. Na Mpigapicha Wetu**

## Mbio Ligi Kuu Zanzibar kati ya KVZ, KMKM yazidi kunoga

**Inatoka Uk.24**

Akiwa kama mtaalam aliyempitisha mtaalam mwingine kutoka Ubelgiji aje afundishe Taifa Stars, pia atakubaliana na wazo la kitaalam la kumwezesha kocha huyo ili awaone wachezaji wetu wa sasa kwa uwanda mpana zaidi.

Wapo kina Clement Mzize huko katika timu za mikoani, kocha atawaona na kushauri nini kifanyike.

Wapo akina Mohamed Hussein na Shomari Kapombe ambao wana uzoefu wa mechi za kimataifa lakini hata hivyo hawajajumuishwa akiwemo, Mzize katika kikosi kilichoitwa kwenda Uganda kuikabili timu ya taifa ya Uganda kwenye michuano ya AFCON.

Kocha Marcio Maximo alimuona Marehemu Godfrey Bony, akiwa ameshacheza Prisons kwa misimu mitano na akacheza mpira mkubwa alipomuita Taifa Stars.

Wapo nyota chipukizi wengine wengi tu tena umri unawaruhusu katika hizi hizi timu za Ligi Kuu zenye kuonekana kama vile zinawasindikiza wakubwa watatu wa Dar. Uzoefu wa kocha, Amrouche wa kufanya kazi katika ukanda huu wa Afrika na utumike hapa kwetu pasipo kuletewa mizengwe ya kumchagulia wachezaji kama vile hana utaalam wa kuwaona yeye mwenyewe.

Aje kulaumiwa siku tukifungwa mechi moja Uwanja wa Benjamini Mkapa kwa makosa yake ya ufundi wa uwanjani. Huku nje awe ameshapewa kila kitu chenye kumrahisishia kazi. siwe timu atakayoifundisha imepenyezwa wachezaji wengi wenye ukaribu na makocha wazalendo wakiwa ni marafiki wanaojuana kwa muda mrefu, halafu akazungukwa na hao hao wakimtaka afungashe virago aondoke zake.

Wachezaji walioitwa kuikabili Uganda ni Aishi Manula na

Beno Kakolanya, (Simba), Metacha Mnata, Kibwana Shomari, (Yanga) na Datius Peter, (Kagera Sugar) na Yahya Mbegu (Ihefu).

Wengine ni David Luhende, (Kagera Sugar), Dickson Job, Bakari Mwamnyeto, Ibrahim Bacca na Mudathir Yahya (Yanga),

Abdallah Mfuko, (Kagera Sugar) Sospeter Bajana, (Azam FC) na Mzamiru Yassin, (Simba)

Wachezaji wengine ni Yusuph Kagoma, (Singida Big Stars), Ramadhan Makame, (Bodrumspor-Uturuki), Abdul Suleiman, (Azam FC), Edmund John, (Geita Gold) na Feisal Salum, (Yanga).

Wengine Khalid Khabibu, (KMKM FC), Anuary Jabir, (Kagera Sugar), Simon Msuva, (Al-Quadsiah-Saud Arabia),

Mbwana Samatta, (KRC-Genk- Ubelgiji), Novatus Dismas, (Zulte Waregem-Ubelgiji) na Alphonce Mabuta, (FK Spartak Subotica-Serbia), Pia wamo Kelvin John, (KRC Genk ya Uelgiji), Ben Starkie, (Bastford United ya Uingereza), Haji Mnoga, (Aldershot Town ya Uingereza), Ally Msengi, (Swallows ya Afrika Kusini), Himid Mao (Ghazi El Mahalla-Misri) na Said Khamis (Al-Fujairah-UAE)

## KVZ netiboli yapongezwa kufanya vyema

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya netiboli ya Kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ), imepongezwa kwa kufanya vyema katika mashindano mbalimbali ndani na nje ya Zanzibar. Pongezi hizo zilitolewa na Kamanda Mkuu wa Kikosi hicho, Luteni Kanali Said Ali Juma Shamhuna alipozungumza na mwandishi wa habari hizi ofisini kwake Mtoni Mkoa wa Mjini Magharibi. Alisema kikosi hicho, awali kilikua hakifanyi vizuri, lakini kwa sasa kimechukua ubingwa wa Zanzibar mara mbili mfululizo na kuchukua ubingwa wa Kombe la Mapinduzi. Luteni Shamhuna alisema, hatua hiyo ni nzuri kwake na matarajio yake kitaendelea kufanya vizuri katika mashindano yote ambayo watakua wakishiriki. Kamanda huyo alisema, mbali na kuchukua ubingwa katika mashindano ya ndani lakini pia walishika nafasi ya pili kwenye Kombe la Muungano na kupata nafasi ya kushiriki michuano ya Afrika Mashariki, ambayo yatafanyika nchini Kenya.



## Amri Saidi Sijawahi kukatishwa tamaa kufundisha soka

Uk. 21

Leo yetu ndiyo kesho yetu

# Mwelekeo Spoti

| Jumanne Machi 15 - 21, 2013 |



## Conte mbioni kuondoka Tottenham Spurs

Uk. 22

# Simba yatamba kwenda nusu fainali Klabu Bingwa

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZU wa Klabu ya Simba umesema, Jumamosi wanakwenda uwanji wakiwa na Kauli mbio ya 'Kuvunja mwiko kuelekea nusu fainali' ambapo safari itaanzia Uwanja wa Benjamini Mkapa dhidi ya Klabu ya Horoya ya Guinea katika mechi ya Klabu Bingwa Afrika Kundi C.

Akizungumza Dar es Salaam jana Meneja wa Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally alisema awali malengo yao yalikua ni kufika nusu fainali ambako katika hatua hiyo wanatambua kwamba watakutana na timu kubwa na zenye ubora. Alisema kufungwa na timu kubwa kama Wydad Casablanca kuna jambo la kujifunza, tofauti na kufungwa na timu ndogo ambayo baada ya kufungwa mtu unaanza kujuta umefungwaje na timu isiyokua na ubora.


Ahmed alisema wamepani kucheza nusu fainali na wamejiandaa kucheza na timu kubwa hivyo wanazikaribisha timu kama Waydad na nyingine ambazo zinatamba barani Afrika.

Meneja huyo alisema maandalizi yao yanakwenda vizuri isipokua watamkosa mshambuliaji wake, Augustine Okra ambaye ni majeruhi na pia walikua wakisubiri ripoti ya daktari kuhusu beki wake, Mohamed Otara kama atakua vizuri ataingizwa kwenye kikosi.

"Habari njema ni kumuona, Kibu Denis akirejea tena uwanjani kwa kuwa katika mechi ya Jumamosi ana umuhimu wake ambao kila mmoja anaujua anapokua uwanjani," alisema Meneja huyo.

Alisema mashabiki wanatakiwa kushangilia mwanzo mwisho kwa kuwa mechi ya Jumamosi si ya kinyonge bali ni fainali kwao ya kuvuka hatua ya nusu fainali.

Ahmed kizuri wachezaji wake wanajua umuhimu wa kushinda mechi hiyo na wamepania kuwanyoa Horoya na kujiwekea mazingira mazuri ya kusonga mbele.



**Nahodha wa timu ya Simba, John Bocco akiruka kwanja la mmoja wa mabeki wa Raja Casablanca katika moja ya mechi ya Klabu Bingwa iliyochezwa Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam, ambapo wawakilishi hao walifungwa mabao 3-0. Simba Jumamosi itakutana na Horoya katika mwendelezo wa michuano hiyo itakayochezwa Uwanja wa Mkapa. Picha na Mtandao**

# Wachezaji Yanga, Simba watakiwa kutobweteka

**Na Mwandishi Wetu, Chalinze**

WACHEZAJI wa Klabu za Yanga na Simba, wametakiwa kutobweteka kwenye mechi zao watazocheza mwishoni mwa wiki kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Jumamosi Simba itangulia kucheza na Horoya katika michuano ya Klabu Bingwa Afrika hatua ya makundi Kundi C ambapo katika kundi hilo Simba inashika nafasi ya pili kwa kuwa na pointi sita nyuma ya Raja Casablanca yenye pointi 12 huku huku Horoya ikishika nafasi ya tatu ikiwa na pointi nne.

Nayo Yanga itaingia katika uwanja huo kuikabali Real Bamako ya Mali katika mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi Kundi D ambalo Yanga inashika nafasi ya pili ikiwa na pointi 7 nyuma ya US Monastir inayoongoza kundi hilo.

Rai hiyo imetolewa na mashabiki wa klabu hizo walipozungumza na mwandishi wa habari hizi, ambapo waliwataka kutojiamini kupita kiasi katika michezo yao ya nyumbani badala yake waichukulie kama fainali.

"Mmoja wa mashabiki hao Juma Chuma, mwanachama wa Yanga Chalinze alisema," tuna timu nzuri lakini katika kuelekea mchezo wetu wa mwishoni mwa wiki hii niwatake wachezaji wetu, wasiuchukulie poa badala yake wacheze kwa bidii na wasiwe na papara," alisema Chuma.

# Mizengwe majina ya wachezaji Stars na uzoefu wa Amrouche

**Na Mwandishi Wetu**

YAPO malalamiko ya muda mrefu kuhusu majina ya wachezaji wa timu ya taifa 'Taifa Stars' yanavyopatikana. Ni ya chini chini yanayosikika miongoni mwa wadau wa mpira. Kila kocha wa Stars anapotangaza wachezaji kwa ajili ya mechi inayofuata, watu wanatazama usoni na miguno inasikika. Maswali ya kwa nini wachukuliwe wachezaji wachache tena wale wa Yanga, Simba na Azam huwa yanasikika sana.

Mchezaji anacheza Tanzania Prisons mwaka mmoja anachukuliwa na Kagera Sugar anakaa huko misimu miwili. Anapokuja tu Yanga au Simba, inakua ni tiketi ya kwanza ya safari ya kuvaa jezi ya Taifa Stars.

Wajuzi wa mpira wanaozeekea katika maongezi ya vijiweni wanauliza mara kwa mara, huu ubora wa mchezaji unaifaa timu ya taifa pale anapochaguliwa tu kuchezea Yanga au Simba?

Ni hapo inapozaliwa dhana inayosikika midomoni mwa watu kwamba uteuzi wa majina ya wachezaji wa Taifa Stars, inazingatia mambo mengi ya kibinafsi hasa miongoni mwa makocha wanaomsaidia Kocha Mkuu.

Wao wanabebeshwa lawama wakiwa ni walimu wazalendo wanaokulia katika hizi timu wakizifundisha maisha yao yote. Na makocha wakuu ni watu wa mshahara tu. Wanaofanya kazi kwa mikataba na ikirefushwa sana itamchukua kocha miaka mitano. Ugeni wa makocha wa kigeni unatumika katika kumpatia majina ya wachezaji wanaotiliwa shaka na watu walio karibu na mpira.

Tumekua tukipoteza vipaji kwa miaka mingi kwa kuendeleza hii hulka ya kujuana, kati ya makocha na wachezaji wanaowavutia.

Pale England, mechi inachezwa uwanjani na kamera ikisogezwa majukwaani anaonekana Kocha Mkuu wa timu yao ya taifa, akiwa makini kuangalia kipaji kipi kipya kinajitokeza. Anakua na uhuru mpana wa kuchagua wachezaji anaowataka na ukitazama uwezo wa majina ya wachezaji wanaoitwa, unagundua kuwa kwa wakati huo ndiyo vipaji halisi vyenye haki ya kuchaguliwa.

Akiitwa Ben White kule upande wa beki wa kulia ni kweli anakua katika fomu kuwazidi wachezaji wengi wanaocheza nafasi yake. Akiitwa Marcus Rashford, una uhakika kabisa ni mshambuliaji mwenye fomu ya juu wa wakati huo. Hiyo ni kazi ya miezi kadhaa inayofanywa na Kocha Mkuu Gareth Southgate, akisaidiwa na makocha wengine tena baada ya mjadala wa kina kabla hajatangaza wachezaji wapya.

Harry Maguire, alionekana kama atakua uchochoro kule Qatar katika fainali ya michuano ya Kombe la Dunia, lakini hakufanya makosa makubwa ya wazi katika mechi zote alizocheza. Maamuzi ya makocha yalifanyika kitaalam na yakawa sahihi. Wanakuja makocha wa kigeni kufundisha Taifa Stars na watu wa mpira wanarudia tena na tena kufikisha ushauri wao kwa uongozi wa TFF, kwamba ni vyema Kocha Mkuu mpya Adel Amrouche akazunguka mwenyewe na kutazama wachezaji wetu wanaozidi kukua.

Ameletwa nchini baada ya Oscar Milambo na wasaidizi wake, kujiridhisha kuwa anatufaa kwa aina ya mkwamo tulionao kwa sasa.

Na Milambo ni kocha mwenye shahada inayoheshimiwa huko Ulaya na duniani kwa ujumla.

**Inaendelea Uk.23**